UKIOKOTA RUDISHA KWA: ______________________________ SIMU: ______________

*Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea©*

# Safari
# HATUA 1

Mishale 3 (3 Arrows) — v3.1 (2024)

## Vituo vya Mapumziko, Mwongozo wa Safari, Zana za Huduma

***Strategic Impact***

**S.L.P. 78640, Dar es Salaam, Tanzania**

www.StrategicImpactInternational.com

© Haki miliki, Strategic Impact. Hakuna mabadiliko yanayoruhusiwa kwenye kitabu wiki, lakini unaweza kutoa nakala na kuwagawia wengine bila kubadili yaliyomo.

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

# *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*©

# *Safari* - HATUA 1

## Yaliyomo


***SI Ramani ya Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*** 3
***Strategic Impact Maelezo Kwa Ufupi*** 4
***Hatua 10 za Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*** 5
***Ramani ya Huduma ya Strategic Impact*** 6
***Maswali ya ya Kukua Kiroho*** 7
**Mchakato wa *Safari ya Timu*** 8

**HATUA 1 - *Kituo cha Mapumziko, Mwongozo wa Safari*, wa Zana za Huduma**

*Kituo cha Mapumziko 1* - Upendo Wako wa Kwanza 11
*Kituo cha Mapumziko 2* - Utambulisho Wako Ndani ya Kristo 13
*Kituo cha Mapumziko 3* - Kipaumbele Chako cha Kwanza 15
*Kituo cha Mapumziko 4* - Ufanye Ujumbe wa Injili Kuwa Rahisi 17
**Zana** kwa *Kituo cha Mapumziko 4 - Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* 19-22
*Kituo cha Mapumziko 5* - Ushuhuda Wako Binafsi 23
*Kituo cha Mapumziko 6* - Kipaumbele cha Upendo 25
*Kituo cha Mapumziko 7* - Mtindo Wako wa Maisha ya Uinjilisti 27
*Kituo cha Mapumziko 8* - Msingi wa Biblia 29
*Kituo cha Mapumziko 9* - Ukiri wa Dhambi na Ushirika na Watu Wengine 31
*Kituo cha Mapumziko 10* - Kuwafanya Wanafunzi Waliokomaa na Wanaojizidisha 33
*Kituo cha Mapumziko 11* - Kushirikiana na Roho Mtakatifu kwa Njia Sahihi 35
*Kituo cha Mapumziko 12* - Muhimu kwa Kuwafundisha Wengine 37
**Zana** kwa *Kituo cha Mapumziko 12 - Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI* 40-41
*Kituo cha Mapumziko 13* - Ubwana wa Yesu 42
*Kituo cha Mapumziko 14* - Wakati Wako Peke Yako na Mungu 44
*Kituo cha Mapumziko 15* - Jinsi ya Kujifunza Biblia 46
**Zana** kwa *Kituo cha Mapumziko* 15 - *Zana ya Kukisomea Biblia Peke Yako* 48-50

**Kwa Matumizi Yako** - Jisikie huru kuzalisha tena Zana hizi kwa ajili ya matumizi ya uinjilisti na ufuasi
*Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* 51-52
*Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI* 53-54

*Hatua 1* kwa Ufupi 55

## SI Ramani ya Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea

| *Hatua* | Muhusika | Marudio | Mafunzo/Zana | Muda |
|---|---|---|---|---|
| **1 *Safari ya Maisa Wako*** kuwafanya wanafunzi waliokomaa na wanaoweza kujizidisha | **Wakristo WOTE** | **Endelea kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha hadi Kizazi cha 4.** | **Matukio ya Kuingia**<br>***-Uzinduzi wa Wanafunzi Wanaojizidisha (MDL) au***<br>***-Uzinduzi wa Kiongozi (LL) au***<br>***-Safari Hatua 1***<br><br>**Zana za Huduma**<br>***-Safari Hatua 1***<br>***-Ramani ya Huduma*, -Mwongozo wa Safari, *-Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI* and *Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI*** | **-Siku 1 MDL or**<br>**-Siku 3 LL**<br>**-Miezi 4-6 mafunzo ya *Safari Hatua 1***<br>**-Safari ya Maisha ya kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha** |
| **2** *Safari ya Maisha Wako* kupanda na kukuza Makanisa yanayojizidsha | Wakristo WENGI | Endelea kupanda na kukuza makanisa yanayojizidisha hadi Kizazi cha 4. | *-Matukio ya Mafunzo ya SI*<br>*-Safari Hatua 2*<br>*-Zana za Huduma za SI* | -Siku 1-3 matukio ya mafunzo<br>-Miezi 4-6 mafunzo ya *Safari Hatua 2* |
| **3** *Safari ya Maisha Wako* ya viongozi wapanda makanisa yanayozidisha | BAADHI ya wakufunzi wa wapanda makanisa | Endelea kutambua na kufundisha viongozi/ wapanda makanisa wanaojizidisha hadi Kizazi cha 4. | *-Matukio ya mafunzo ya SI*<br>*-Safari Hatua 3*<br>*-Zana za Huduma za SI* | -Siku 1-3 matukio ya mafunzo<br>-Miezi 4-6 mafunzo ya *Safari Hatua 3* |
| **4** *Safari ya Maisha Wako* kutumika kwenye *Timu Inayojizidisha kuunda eneo jingine* | Viongozi Wachache kwenye timu ya mahali ya *Strategic Impact* | Endelea kutumika kwenye timu inayojizidisha kwenye eneo jingine (kitongoji, kijiji, mji). | *-Matukio ya mafunzo ya SI*<br>*-Safari Hatua 4*<br>*-Zana za Huduma za SI*<br>-Kongamano la viongozi la mwisho wa mwaka *(Fan-the-Flame Leadership Summit)* | -Siku 1-3 matukio ya mafunzo<br>-Miezi 4-6 mafunzo ya *Safari Hatua 4* |
| **5** *Safari ya Maisha Wako* kuanzisha na kuongoza MITEMBEO INAYOJIZIDISHA | Chagua viongozi wachache wa *Strategic Impact* katika kanda wenye uwezo wa kuanzisha mitembeo | Endelea kuanzisha mitembeo ya makanisa yanayojizidisha katika nchi na kanda mpya. | *-Matukio ya mafunzo ya SI*<br>*-Safari Hatua 5*<br>*-Zana za Huduma za SI*<br>-Kongamano la viongozi la mwisho wa mwaka *(Fan-the-Flame Leadership Summit)* | -Siku 1-3 matukio ya mafunzo<br>-Miezi 4-6 mafunzo ya *Safari Hatua 5* |

**UNACHOTAKIWA KUKIFANYA ILI KUTIMIZA AGIZO KUU NI KUENDELEA KUJIZIDISHA KATIKA VIWANGO VYOTE HADI KIZAZI CHA 4.**

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

# *Strategic Impact Kujizidisha*

***Viongozi ✢ Wanafunzi ✢ Makanisa ✢ Harakati***

## UTAMBULISHO:

**Sisi ni viongozi wenye mtazamo wa aina moja wa mtembeo, wenye mzigo na kujitoa kwa Yesu Kristo na kwa kila mmoja wetu ili kutimiza Agizo Kuu.**

## MAONO:

**Tupo ili kumpa kila mtu tumaini pekee la uzima wa milele katika Yesu Kristo katika maisha yetu, au kufa tukijaribu.**

*"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* - Mathayo 28:18-20

## MALENGO:

Tunawafundisha viongozi watakaozidisha wanafunzi watakaowasha moto wamtembeo wa upandaji wa makanisa kila mahali.

*"...na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi hayo ukawakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* - 2 Timotheo 2:2

## MKAKATI:

Tunatengeneza timu za viongozi kimkakati kwenye miji ya ulimwengu ili kuzidisha mtembeo wa kupanda makanisa katikati ya kila kundi la watu.

*"(Paulo) akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia walisikia neno la Bwana."* - Matendo 19:9-10

## MCHAKATO:

***Semina ya Maono* (VS)**

"Kuona Agizo Kuu."

*Utambulisho wa siku moja wa Strategic Impact.*

***Uzinduzi wa Wanafunzi Wanaojizidisha* (MDL)**

"Kupata Uzoefu wa Agizo Kuu."

*Maono ya mafunzo ya vitendo yakuwafanya wanafunzi wanaojizidisha.*

***Uzinduzi wa Kiongozi* (LL)**

"Kujifunza Agizo Kuu."

*Kupata uzoefu mkubwa wa kukua binafsi katika uongozi, na upandaji wa makanisa.*

***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* (SAFARI)**

"Kuliishi, Kuliongoza, na Kuzindua Agizo Kuu."

*Safari ya Maisha Kuufikia Ulimwengu Wako Ulipoptea kwa njia ya kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha, makanisa, viongozi na mitembeo..*

***Mafunzo Mahususi ya Kiongozi* (LIT)**

"Kukua Katika Agizo Kuu."

*Kupata uzoefu mahususi kwa wale waliokwenye Safari ya kukua katika tabia ya uongozi na ubobezi wa uongozi kwa ajili ya Agizo Kuu.*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

# HATUA 10 ZA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA (V3.0)

## HATUA 1: BADILI KUFIKIRI KWAKO

*BADILI FIKRA toka hwenye malengo ya "kulijenga kanisa langu" waza "kuifikia jamii yako iliyopotea → nchi →dunia."*
*(Mathayo 28:18-20; Matendo 1:8; Matendo 20:24)*

## HATUA 2: OMBA

*OMBEA watenda kazi kwa ajili ya mavuno! (Luka 10:2; Matendo 13:1-3)*

## HATUA 3: TANGAZA MAONO

*Eleza MAONO ya Mungu kwa watu wake juu ya kulifikia eneo lako kwa ajili ya kueneza Injili. (Matendo 1:8; 13:1-3)*

## HATUA 4: KUSANYA NA UANDAE TIMU

*Tambua, chagua, KUSANYA NA UANDAE TIMU ya angalau watu wawili wapanda makanisa kila mwaka. (Matendo 14:21-28; 19:9-10; Wakolosai 1:7; 2 Timotheo 2:2)*

## HATUA 5: CHAGUA MAHALI

*KWA NJIA YA MAOMBI CHAGUA MAHALI au kikundi cha watu wa Mungu ambao Mungu anakuongoza kuwafikia kwa Injili. (Matendo 16:6-40)*

*A. TAMBUA mahali ambapo Roho Mtakatifu anakuongoza kuanzisha kanisa la nyumbani..*

*B. TAFITI MAHITAJI yao, ngome zinazotawala, na shughuli za eneo hilo ambazo zinaweza kuathiri hilo kanisa jipya au uliyoanzisha.*

## HATUA 6: FANYA UNJILISTI

*WAHUBIRIE WATU waliopo katika hilo eneo. (Matendo 5:42; 14:21,25; 20:20)*

## HATUA 7: WAFUNDISHE WANAFUNZI WAPYA WALIOAMINI

*WAFUNDISHE waamini wapya mahali au katika eneo lao ulilowakuta.*
*(Matendo 14:22; 20:20)*

## HATUA 8: WAKUSANYE WAAMINI WAPYA

*KUKUSANYA waumini wapya pamoja kwa vipaumbele vinne vya huduma ya kanisa:*

*A. Kuabudu (Matendo 2:42-43; 1 Corinthians 14:26-35; 16:1-2; Wakolosai 3:16),*
*B. Ukuaji (Matendo 2:42; Wakolosai 4:16; 2 Timotheo 4:2),*
*C. Ushirika (Matendo 2:44-46; 8:35-38; Waefeso 4:11-16),*
*D. Unjilisti (Matendo 2:47; 5:42; 8:4; 19:10; Wafilipi 2:15-16).*

## HATUA 9: ZIDISHA WANAFUNZI


*ZIDISHA wanafunzi walio katika kanisa jipya kwa kurudia tena hatua hizo 8 za mwanzo. (1 Wathesalonike 1:7-8)*

## HATUA 10: FUNGAMANISHA MIKONO PAMOJA ILI KUZINDUA MTEMBEO

*FUNGAMANISHA mikono na viongozi wengine kuzindua mtembeo wa kuzidisha wanafunzi ili kutimiza Agizo Kuu.*

***www.StrategicImpactInternational.com***

# RAMANI YA HUDUMA



## *Strategic Impact*
## *Maswali ya ya Kukua Kiroho*

Maswali haya yamekusudiwa kukusaidia wewe kukua katika ibada yako na Kristo, uhusiano wako na Yeye, katika tabia ya kiungu, na uaminifu katika kujitoa. Tutakuwa pamoja kwa njia ya kuungama dhambi kwa Mungu na kwa sisi kwa sisi kama wanafunzi wanaowajibika kila mtu kwa mwenzake (1 Yohana 1:9; Yakobo 5:16; Waefeso 4:25; Wagalatia 6:1). Maswali haya yaulizwe na kujibiwa kwa uaminifu kwa neema na kwa usiri katika roho ya upendo wa kweli. **HUU SI** wakati wa kuhukumiana (Warumi 8:1) bali wa kutiana moyo katika kumpenda Mungu, Matendo mema na haki.

*"Lakini tunda la roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole kiasi, juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."*

(Wagalatia 5:22-23)*

**Wiki hii…**

1. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?
2. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano yako na wenzio, majirani na maadui zako?
3. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo? Kwa namna gani?
4. Je umekuwa na kiasi na kumheshimu Kristo kwenye michakato yako ya kifedha?
5. Je umejizuia dhidi ya mawazo ya ngono na matendo yake au je umezoelea tabia yoyote ambayo inaleta vifungo?
6. Je ni nani ambaye **umemuongeza** kwenye *Ramani ya Huduma* mwezi huu?

**Neno kuhusu mambo ya kutekeleza na *Timu yako ya Safari*…**

Munapoendelea kukua na kutumika pamoja kwenye *Timu ya Safari*, munaweza mukawa na mmoja wenu kwenye kikundi ambaye pengine hawezi kutekeleza mambo munayotakiwa kutekeleza kila wiki (usemi wa "Nitafanya", Uinjilisti, kuwafunza wengine, na kusoma Biblia). Hii inaweza kutokana na majukumu mengine ya kimaisha aliyonayo au ni tabia tu ya kutokutekeleza mambo munayo kubaliana katika *Safari*. Kama hivi ndivyo ilivyo tunaliacha jukumu hili kuamuliwa na *Timu ya Safari*. Ushauri wetu ni kwamba mtu anayesuasua kwenye safari apewe wiki 2 au 3 ili kukamilisha mambo muliyokubaliana kufanya kila wiki, na kama atashindwa kutekeleza mambo anayotakiwa kufanya kwa muda aliopewa basi mtu huyo anaweza kuwekwa kando ili *Timu ya Safari* iweze kuendelea bila yeye kuwepo. Watu wa namna hii wanakaribishwa kujiunga na *Timu ya Safari* wakati mwingine huko mbeleni kama wakimaanisha. Watu wanaotimiza Agizo Kuu si watu wenye akili, matajiri au watu waliosisimka tu. Watu wataotimiza Agizo Kuu ni wacha Mungu waliojitoa na walio tayari kumtii Kristo.

***KUMBUKA:** Nukuu zote za Biblia zimetoka kwenye Biblia Takatifu- Tafsiri ya Union Version ya 1952 (United Bible Society).

# *MCHAKATO WA SAFARI YA TIMU*

Karibu kwenye ***TIMU YA SAFARI.*** Dada na Kaka zangu katika Kristo timu yako ya watu 3 hadi 5 ipo kwenye safari ya maisha ya kuufikia ulimwengu uliopotea, kwa kuwapa tumaini pekee la uzima wa milele ndani ya Yesu Kristo. Kama ilivyo kawaida munapoenda safari pamoja, timu yako itahitaji kuchukua ***VITUO VYA MAPUMZIKO*** ya mara kwa mara. ***MAPUMZIKO KATIA SAFARI*** yanatakiwa yatokee kama Mikutano ya kila wiki ya timu ya safari na itachukua muda wa saa moja na nusu. Tumegundua kwamba kupata mapumziko kunatia moyo kujitolea na kuendelea kuwa thabiti. Kila ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kitahusisha ***4 KUANGALIA MAMBO 4*** na ***MASWALI 10*** kitu ambacho kitawasaidia ili mufike munakokwenda pamoja. ***VITUO VYA MAPUMZIKO*** ni muda wa kikundi kugundua mambo — hakuna anayefundisha, lakini kila mmoja kwenye timu atajifunza kwa mwenzake mutakapokuwa munasoma sura za Biblia na kisha kujadiliana na kujibu maswali.

1. **ANGALIA NYUMA —** Kama ilivyo katika safari yoyote kuna faida kuangalia namna mulivyoendelea na safari kutokea kwenye ***KITUO CHA MWISHO CHA MAPUMZIKO***. Kuangalia Nyuma kunahusisha maswali matatu ya kwanza ya kujadiliana yenye mkazo juu ya:
   - Ukuwaji wa tabia na maisha yako ya kiroho ndani ya Kristo (**SWALI 1**),
   - Namna ulivyotunza ahadi ya mambo ya kutimiza kufanya wiki hii kwenye ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kilichopita (**SWALI 2**),
   - Watu uliowashuhudia na kuwafundisha wiki iliyopita (**SWALI 3**).

**KUMBUKA**: Haya maswali ya **KUANGALIA NYUMA** ni muhimu sana. ***SAFARI*** yako inahusisha kukua katika maarifa na kumtii Yesu. Kama wanatimu hamutimizi mambo muliyotakiwa kufanya kila wiki, hiyo timu haitakiwi kuendelea mbele inatakiwa irudie masomo yale yale muliyotakiwa kufanya kwenye ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kilichopita.

2. **ANGALIA JUU** — Timu yako itamwangalia Mungu juu kwenye Biblia ili kujifunza jinsi ya kukua wakati mukiwa safarini. Mutajadiliana maswali mawili kila wiki kutegemea sura mahususi ya kwenye Biblia ***SAFARINI***. **SWALI 4** Ni kitu gani ambacho umekipenda au umeona kimekutia moyo kwenye sura hii? **SWALI 5** *Ni kitu gani kinacho kuchanganya au kinakufanya ukose raha kwenye maandiko haya?*

3. **ANGALIA NDANI** — Kuangalia ndani kunahusisha **MASWALI 6** na **7**, ambayo yanahusiana na kweli maalumu ya vifungu vya Biblia. Maswali haya yatakusaidia kufikiri jinsi gani utaitumia kweli ya Biblia ambayo munaijadili baada ya maswali ya **KUANGALIA NDANI**, timu yako kwa pamoja mutasoma ukurasa mmoja wa ***MWONGOZO WA SAFARI***. This ***MWONGOZO WA SAFARI*** utasaidia kufafanua ***KWELI YA MSINGI*** ya vifungu vya Biblia.

4. **ANGALIA MBELE — SWALI LA 8** litakuongoza kuandika kitu maalumu **utakachofanya** ili kutii kweli ya Biblia wiki hii. Kwenye **SWALI 9** utaorodhesha **nani** utawashuhudia habari za Yesu au kuwafundisha kwa wiki inayokuja na mjadiliane wewe na *TIMU YA SAFARI* yako munavyoweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kuwafundisha waongofu wapya kabla hamjafika kwenye ***KITUO CHA MAPUMZIKO***. **SWALI LA 10** linauliza vifungu gani vya Biblia ambavyo mutasoma kila siku kwa wiki inayokuja. Tunashauri kiwango cha chini cha kusoma Biblia kila siku kiwe sura 3, ingawa unaweza kusoma zaidi. Utekelezaji wa mambo ya kufanya yaliyopo kwenye **MASWALI** 8, 9, na 10 yatathibitishwa kwenye mikutano kwenye ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

5. **MAOMBI —** Mwisho, mwisho wa ***Kituo cha Mapumziko***, ombeaneni mahitaji yenu na muendelee kuombeana hadi mkutano mwingine kwenye ***Kituo cha Mapumziko*** kinachofuata.

Kila mkutano kwenye ***Kituo cha Mapumziko*** utazingatia mfumo huu — ***Kuangalia Mambo 4*** na ***Maswali 10***. Munapoendelea kukua pamoja na kutii yale ambayo Bwana anawafundisha kutoka kwenye Biblia kwenye ***Hatua 1*** ya ***Safari***, mutajengwa na kuhusika katika kuendelea kuzidisha wanafunzi kwenye ***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea***.

***Kituo cha Mapumziko*** cha kwanza kinaanza kwenye ukurasa unaofuata. Mungu akubariki sana unapoanza ***Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea***.

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

*Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea©*

# Safari
# HATUA 1

## Vituo vya Mapumziko, Mwongozo wa Safari, Zana za Huduma

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 1 - *UPENDO WAKO WA KWANZA*

**TIMU WATU 3-5** **KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10** **15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?

2. (**KUMBUKA**: Kwenye kila *KITUO CHA MAPUMZIKO* katika *SAFARI* kipindi kinachofuata utaulizwa. Je, ulikuwa mwaminifu ukisoma Biblia na ukitimiza AHADI zako wiki hii?)

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata. Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Ufunuo 2:1**-**7** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Ufunuo 2:1**-**7** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Ni huduma au shughuli gani za kidini ambazo unafanya zinazochukua nafasi ya ushirika wa upendo wako kwa Yesu?

7. Ni mambo gani ya vitendo yaliyokusaidia kukuza ushirika na upendo wako wa kwanza kwa Yesu?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 1* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Ufunuo 2:1**-**7** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA______________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ______________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 1 - *UPENDO WAKO WA KWANZA*

Yesu alieleza wazi wazi katika Mathayo 22 :37-40 kitu ambacho Mungu anataka zaidi kutoka kwetu: *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako, katika amri hizi mbili hutegemea Torati yote na Manabii."*

Zaidi ya yote Mungu anataka umpende Yeye na kila kitu kilicho ndani yako. Hili ni jambo la kushangaza- Mwenyezi Mungu wa milele, Muumbaji anatamani ushirika wa upendo na wewe.

Mungu hakulalamika juu ya wana wa Israel kufanya shughuli za kidini au kutoa dhabihu. Malalamiko yake ni kwamba walibadilisha ibada yao ya upendo kwaYeye na hivyo vitu (Angalia Zaburi 40:6-8; 50:7-17). Hasira yake ikawaka kwa sababu ya ibada zao za sanamu, kubadili ibada yao kwa Mungu na vitu vingine (angalia Ezekiel 6:9)

Katika Ufunuo 2 :1-7 Yesu analisifia kanisa la Efeso kwa bidii yao katika kazi, uvumilivu, usafi, kukosoa imani potofu na kuteswa kwa ajili yake. Hili lilikuwa ni kanisa zuri sana. Hata hivyo Yesu aliwakemea kwa kuwa walipoteza upendo wa kwanza (mstari 4). Anawaambia watubu na kurejea kwenye ushirika wa upendo wa kwanza na Yeye (pamoja na wengine), au angeondoa kinara cha taa juu yao, ambayo ndo kanisa lao (mstari 6 angalia pia ufunuo 1:20) Yesu anawaambia waona wewe – kwamba ni bora asiwe na kanisa kuliko kuwa na kanisa zuri lakini lisilo na upendo.

Wote tunakabiriwa na hatari ya kubadili upendo wetu kwa Mungu na kuweka huduma kwanza. Mara nyingi watu wanafurahia vyeo au nafasi, utajiri na nguvu (Madaraka) – hata ndani ya kanisa! hata hivyo Mungu anafurahishwa na moyo ambao umejaa ibada kwa ajili yake (Zaburi 40:6-8). Mungu anatafuta mahusiano ya karibu yenye upendo na wewe kuliko ibada unayoifanya kwake.

Mahusiano ya upendo unaokuwa na Yesu ndiyo chanzo cha kila kitu kwenye maisha yako. Motisha wa aina nyingine yoyote utashindwa. Upendo wako kwa Yesu ndiyo kitu pekee kitakachokufanya upite kwenye magumu yenye kukatisha tamaa salama. Upendo wako kwa Yesu ndio kitu pekee kitakacho kufanya wewe uwapende watu wengine. Upendo wako kwa Yesu ndo kitu pekee kitakachokufanya uwashirikishe Injili watu waliopotea.Upendo wako kwa Yesu ndo kitu pekee kitakachokufanya uhamasike kutimiza Agizo Kuu. Upendo wako kwa Yesu ndo kitu pekee kitakachokusaidia kushinda majaribu na mateso. Yesu alisema, mkinipenda, mtazishika amri zangu (Yohana 14:15). Kutoka kwenye moyo wa upendo utii unatiririka.

**KWELI YA MSINGI**: MUNGU ANATAKA WAFUASI WALIOJITOA KIKAMILIFU KUMPENDA YESU KWELI YA MSINGI .

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

## HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 2 - *UTAMBULISHO WAKO NDANI YA KRISTO*

**TIMU WATU 3-5** **KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10** **15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano yako na wenzio, majirani na maadui zako?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata. Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Warumi 8:14-16** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Warumi 8:14-16** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Muulize Mungu; "unawaza nini juu yangu?" andika chochote ambacho Mungu amesema na wewe.

7. Muulize Mungu. "Mimi ni Nani?" Andika chochote ambacho Mungu amesema na wewe.

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 2* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Warumi 8:14-16** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 2 - *Utambulisho Wako Ndani ya Kristo*

Wewe ni nani? Kwa nini unaishi? Ukijibu kwa usahihi maswali haya mawili maisha yako yatakuwa ya maana na ya thamani. Kutokujua majibu ya haya mswali kutapelekea kukata tamaa na kuvunjika moyo.

Lakini majibu ya maswali haya yatatoka wapi? Jamii na utamaduni wako vinajaribu kutoa majawabu. Watu wengine pia wanajaribu kukushawishi na kukufafanua wewe ili uishi kwenye utambulisho na makusudi wanayokupa. Kwa maana nyingine wengi wanajaribu kutafiti ndani yao ili kugundua utambulisho wao wa kweli na makusudi ya maisha yao. Lakini hakuna chanzo chochote katika hivi kinachotoa majibu yanayotosheleza naya kweli kwamba wewe ni nani na kwa nini unaishi.

Chanzo cha pekee na cha kweli kinachojua wewe ni nani na kwa nini unaishi ni Yeye aliyekuumba na kukuokoa, Mungu mwenyewe: *"Maana wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu uliniunga tumboni mwa mama yangu"* (Zaburi 139:13). Mungu anajua **utambulisho** wako kwa kuwa ndiye aliyekuumba. Mungu alimwambia nabii Yeremia, *"kabla sija kuumba katika tumbo nalikua na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa, nimekuweka kuwa nabii wa mataifa"* (Yeremia 1:5). Mungu anajua **makusudi** ya maisha yako kwa kuwa hilo ndilo kusudi la Yeye kukuumba wewe.

Kwa sababu hiyo, siyo wewe au mtu mwingine yeyote anayeweza kuelezea utambulisho wako wa kweli. Siyo wewe au mtu mwingine yeyote anayeweza kueleza kusudi la kuumbwa kwako. Unaweza tu **kupokea** utambulisho na kusudi ulilopewa na Mungu.

Unapokea utambulisho Kama mwana/ binti wa Mungu wakati Roho Mtakatifu kwa uwezo wa kiungu anapougeuza moyo wako kwa njia ya kumwamini Yesu. Hili si jambo ambalo unaweza ukarifanya kwa uwezo wako mwenyewe. Unaweza ukapata "uelewe/ufahamu wa kiroho" wa wewe ni nani na kwa nini unaishi wakati Roho Mtakatifu akipandikiza ufunuo huu kwako.

Paulo anaomba kwa ajili yako ili kupata ufunuo wa kiungu katika ufahamu wa kiroho juu ya Mungu: *"… Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya … Ufunuo katika kumjua yeye. Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru mjue…"* (Waefeso 1:17-18a). Unaweza **kujijua** wewe ni nani kwa kuwa Mungu amekwisha kusema kwenye Biblia yake. Lakini utaelewa tu wewe ni nani na kwanini unaishi tu wakati **unapokea** ufunuo huu wa kitambulisho chako na kusudi la kuumbwa kwako kwa Imani.

Kabla ya kumpokea Kristo, ulikuwa yatima wa kiroho. Lakini wakati ulipookoka, Mungu alikuchukuwa wewe ili uwe "mwana/ binti" yake na akakupa *"roho wa kufanywa mwana"* (Warumi 8:15b) kama matokeo ya kufanywa mwana, sasa unamwita Mungu Aba yaani Baba!

Hata hivyo utaendelea kuishi kama "yatima wa kiroho" mpaka **usikie** na **kukubali** tangazo la Baba la utambulisho wako wa kweli ndani ya Kristo."Wewe ni Mwanangu/ Binti yangu mpendwa! Nimependezwa na wewe **pokea** na **kazia utambulisho** wako wa kweli na kusudi la kuumbwa kwako kwa kumuomba Baba yako wa mbinguni, "Mimi ni nani?" na "Kwa nini ninaishi?" Na kisha uuishi huu utambulisho na kusudi la kuumbwa kwako kwa Imani.

**Kweli ya Msingi**: UTAMBULISHO WA KWELI NA KUSUDI LA KUUMBWA KWAKO VINAWEZA TU KUPOKELEWA KWA KUPOKEA UFUNUO WA ROHO MTAKATIFU; NA SIYO KWA JITIHADA ZA KIBINAAMU.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 3 - *KIPAUMBELE CHAKO CHA KWANZA*

**TIMU WATU 3-5 KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10 15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo? Kwa namna gani?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Mathayo 28:18-20 na 2 Timotheo 2:2** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Mathayo 28:18-20 na 2 Timotheo 2:2** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Kwa nini wachungaji na viongozi wengi wanajishughulisha sana na shughuli za kanisa kuliko kuufikia ulimwengu uliopotea?

7. Jinsi gani utatia mkazo wa kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha hasa kwa kubadili vipaumbele vya huduma yako?

**[Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 3* ukurasa unaofuata.]**

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Mathayo 28:18-20 na 2 Timotheo 2:2** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA______________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ______________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10.Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 3 - *Kipaumbele Chako cha Kwanza*

Wachungaji na viongozi wengi wa kanisa wanaheshimika lakini wamepotoshwa kwa shauku ya kujenga jengo kubwa la kanisa. Wengi wanatafsiri kwamba kuwa na kanisa kubwa ni kuwa na bajeti kubwa na sifa kubwa. Kanisa kama hili laweza kuonekana kuwa kubwa au la mbele ya macho ya Mungu.

Hata hivyo Yesu hajamuita yeyote kati yetu kujenga jengo la kanisa kubwa. Hakuna agizo kama hilo kwenye Biblia au kupanda kanisa, katika Agano Jipya. Jambo muhimu kuhusu kanisa lolote siyo idadi ya watu, Jengo kubwa au ratiba zilizopo. Jambo.

Kama Yesu hakukuita kujenga kanisa kubwa, sasa unatakiwa kufanya nini? Alieleza wazi wazi kwenye Agizo lake la mwisho. Unatakiwa *"Unatakiwa Uende ukawafanye mataifa kuwa wanafunzi…"* (Mathayo 28:19). Hili ndilo Agizo Kuu. Wajibu wako wa msingi ni kupeleka Injili kwa watu, jirani zako, vijijini, mijini na kwa mataifa na kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha ambao nao watauzidisha ufalme Wake. Tunauona huu mfano kwa kanisa la Agano Jipya. Kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume, wakati mitume na wanafunzi wengine walipojikita kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi, makanisa yalianzishwa yalikua na yalijizidisha. (Angalia Matendo 6:1,7; 9:31; 19:10). Makanisa haya yalikuwa na muundo rahisi hata kuweza kujizidisha. Yaliongozwa na viongozi wanaokuwa ambao walijihusisha na Ibada, kuhudumiana wao kwa wao, kufundishana na kuwashuhudia walio nje (1 Timotheo 3, Titi 1; 1 Wakorinto 14, Wakolosai 3:15-17; 4:2-6).

Ndugu katika Bwana ni lazima tubadili kufikiri kwetu juu ya wito ambao Mungu ametuitia kufanya. Jukumu lako la msingi siyo kupanda na kujenga kanisa kubwa bali ni kuwafanya wanafunzi wanaokuwana kujizidisha. Kama hili utalifanya kuwa ndo lengo lako mahususi basi matokeo yake ni kwamba makanisa yanayojizidisha yatatokea.

Agizo la mwisho la Yesu ndilo liwe kipaumbele chako cha kwanza.

**Kweli ya Msingi**: YESU HAKUKUITA WEWE KUJENGA KANISA KUBWA BALI KUWAFANYA WANAFUNZI WANAOJIZIDISHA.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umekuwa na kiasi na kumheshimu Kristo kwenye michakato yako ya kifedha?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **1 Wakorintho 15:1-8** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **1 Wakorintho 15:1-8** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Mistari hii inatufundisha nini ili mtu aokoke na kupata uzima wa milele?

7. Ni jinsi gani Mkristo wanavyowachanganya wengine jinsi mtu anavyoweza kupokea uzima wa milele?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 4* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **1 Wakorintho 15:1-8** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 4 - *Ufanye Ujumbe wa Injili Kuwa Rahisi*

Mungu anataka watu wote waokolewe na kupata kujua yalipo kweli (1 Timotheo 2:4) amekuita wewe ili kushirikiana naye katika uinjilisti huu mkubwa. Maono yetu ni kuona kila mtu anasikia jinsi ya kumjua Yesu tumaini pekee la uzima wa milele.

Katiaka *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea* lazima uendelee kuwashirikisha Injili watu wengine kwenye jamii yako.ni muhimu sana kwamba uielewe Injili ili uwashirikishe wengine kweli, wazi wazi na kwa urahisi ili waje katika Imani ya wokovu Katika Kristo. Tumegundua kwamba wachungaji na viongozi wengine wanapata mkanganyiko juu ya jambo hili muhimu.

Mambo muhimu ya msingi ya ujumbe wa Injili yanapatikana kitabu cha 1 Wakorintho 15:1-8, 51-53:

1. **Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zako**, mstari 3.
   A. Mungu anawapenda watu na anataka watu wote waokolewe na kupata uzima wa milele (Yohana 3:16; 1 Timotheo 2:4).
   B. EveKila mtu ametenda dhambi na kutengwa na Mungu (Warumi 3:23)
   C. Yesu ni mwana wa Mungu pekee asiye na dhambi ambaye amelipa adhabu ya dhambi na yeye pekee yake ndiye njia ya uzima wa milele (Warumi 5:8; Yohana 14:6)
2. **Yesu alizikwa katika mwili**, mstari 4.
3. **Yesu alifufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu**, mstari 5-8
4. **Wale watakaomwamini Yesu kuwa mwokozi wao watasamehewa dhambi na kupata uzima wa milele**, mstari 1-2, 51-53.
   A. Ni kwa njia ya kupokea zawadi ya milele kwa neema ya Mungu kwa njia ya Yesu ndivyo mtu anavyoweza kuokoka. (Waefeso 2:8-9)
   B. Kuiweka Imani (uaminifu) yako kwa Yesu ndiyo njia pekee ya mtu kuokolewa kutoka dhambini na kupata uzima wa milele. (Yohana 1:12; 3:16; Warumi 10:9-10)

*Strategic Impact* imeandaa zana ya uinjilisti ili kukusaidia wewe kuupeleka ujumbe rahisi wa Injili na kuwapa fursa wengine kuweka Imani yao kwa Yesu.

PITIA ZANA HII NA MAELEKEZO YA NAMNA YA KUTUMIA KWENYE UKURASA UNAOFUATA.

**Kweli ya Msingi:** ENDELEA KUTOA UJUMBE RAHISI WA INJILI NA KUWAALIKA WATU WENGI KADRI INAVYOWEZEKANA.

[**Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"**]

**KUMBUKA**: *Zana* kamili *ya Uinjilisti ya Strategic Impact* ukurasa 47-49.
Uwe huru kutoa nakala nyingi uwezavyo (kwa gharama yako mwenyewe) ili kuzitumia kwenye uinjilisti.

**STRATEGIC IMPACT - SAFARI YA MAISHA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA**


# ZANA KWA KITUO CHA MAPUMZIKO 4 - *MISHALE 3 ZANA YA TUMAINI NA MAISHA YA SI*

1. Mfahamu mtu unayetaka kumshirikisha naye kwa kuuliza kuhusu **HADITHI YAO**:
   - Jua kuhusu malezi yao ya kiroho
   - Uliza ikiwa mambo ya kiroho ni muhimu kwao.
   - Uliza ikiwa wanahisi kuwa wana uhusiano mzuri na Mungu au la.
   - Uliza kama wangependa kuwa na uhusiano mzuri (bora) na Mungu.
   - Omba ruhusa ya kumshirikisha HADITHI YAKO (ushuhuda wako). Ikiwa wanakubali:


2. Shirikisha **HADITHI YAKO** (ushuhuda wako) ya:
   - Maisha yako yalivyokuwa kabla ya kumwamini Yesu,
   - JINSI ulivyokuja kuweka imani katika Yesu kama Mwokozi wako,
   - Jinsi maisha yako yalivyo tofauti BAADA ya kumwamini Yesu kwa Wokovu.
   - **Uliza**: *"Je, ungependa kujua jinsi unavyoweza kuwa na uhakika kwamba una uzima wa milele pamoja na Mungu?"*

3. Tumia *ZANA YA MISHALE 3 ZA TUMAINI & MAISHA* ***kujadili*** **HADITHI YA MUNGU** na mtu huyo.
   - Onyesha mistari kutoka **Yohana 3:16-18** na Alama Nne.
   - **Sema**: *"Aya hizi ni baadhi ya zinazojulikana sana katika Biblia na zinatuambia jinsi tunavyoweza kuwa na uzima wa milele pamoja na Mungu. Je, ninaweza kuyajadili na wewe?"*

**Muulize mtu huyo kama angesoma Yohana 3:16-18 kwa sauti.**
- Kuwa mwangalifu ikiwa hawawezi kusoma. Ikiwa wanasema kitu kama, "Sina miwani yangu," basi usome mistari kwa sauti.



4. Onyesha ishara ya **MOYO** (MUNGU) na **useme**:
   - Ishara hii inawakilisha Mungu. **Uliza**:
     - *"Unajifunza nini kuhusu Mungu katika mistari hii?"*
   - Sisitiza kwamba <u>Mungu anapenda kila mtu</u> ulimwenguni. **Uliza**:
     - *"Je, unaamini kwamba Mungu anakupenda?"*
     - *"Mungu alionyeshaje kwamba anaupenda ulimwengu?"* (Alimtoa Mwanawe pekee kwa ajili yetu.)
     - *"Mungu anataka nini kwa kila mtu ulimwenguni?"* (Ili wasipotee bali wawe na uzima wa milele)
   - Ikibidi, rejea mistari inayounga mkono kuhusu upendo wa Mungu kutoka sehemu ya #1 ndani ya zana.



5. Onyesha alama ya **WATU** na **useme**:
   - Ishara hii inaonyesha kwamba watu wametengwa na Mungu na upendo wake. **Uliza**:
     - *"Unafikiri ni kwa nini watu wametenganishwa na Mungu na hawana uzima wa milele pamoja naye?"*
       - Eleza kwamba ni kwa sababu ya dhambi zetu na kutomwamini Yesu, Mwana wa Mungu.
     - *"Ni hatari gani kwetu ikiwa tutaendelea katika dhambi na kutokuamini kwetu?"*
       - Eleza kwamba tutahukumiwa kwa sababu ya dhambi na kutoamini kwetu na hatutakuwa na uzima wa milele.
   - Ikibidi, rejelea mistari inayounga mkono kuhusu dhambi ya watu kutoka kwa nukta #2 ndani ya zana.

**Uliza mtu huyo (au wewe) kusoma mistari mara ya pili.**

6. Onyesha alama ya **MSALABA** na **useme**:



- Ishara hii inawakilisha Yesu, Mwana wa Mungu, na kile alichofanya kwa ajili yetu. **Uliza**:
    - *"Unafikiri ni kwa nini Mungu alimtuma Yesu ulimwenguni?"*
        - Eleza kwamba sababu ilikuwa ni kufa badala yetu kwa ajili ya dhambi zetu.
    - *"Je, tunapaswa kuamini nini kuhusu Yesu ili tupate uzima wa milele?"*
        - Eleza kwamba Yeye ndiye Mwana pekee wa Mungu ambaye hakutenda dhambi kamwe, kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zetu ili tuweze kusamehewa, kwamba alifufuka kutoka kwa wafu na ndiye njia pekee ya kupata uzima wa milele pamoja na Mungu.
- Ikibidi, tumia mistari inayounga mkono kuhusu Yesu kutoka sehemu #3 ndani ya zana.

7. Onyesha **ALAMA YA SWALI** (UAMUZI WAKO) na **useme**:



- Kila mtu ana uamuzi kuhusu Yesu na zawadi ya uzima wa milele ambayo Mungu hutoa. **Uliza**:
    - *"Kulingana na mistari hii unapaswa kufanya nini ili kuwa na uzima wa milele pamoja na Mungu?"*
        - Ni lazima tuamini (kuweka imani yetu) katika Yesu kama aliyekufa badala yetu ili kusamehe dhambi zetu na ndiye njia pekee ya kupata uzima wa milele.
    - *"Unafikiri inamaanisha nini kuamini (kuweka imani yako) katika Yesu?"*
        - Kubali kwamba hii ni kweli.
        - Amini kwamba Yesu ndiye njia pekee ya kupata uzima wa milele.
        - Binafsi mtegemee Yesu pekee ili kumjua Mungu na kupata uzima wa milele.
    - *"Uamuzi wako ni upi? Je, ungependa kuweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi yako na kukupa uzima wa milele?"*
        - Wakisema "Ndiyo," waongoze kupitia maombi ya imani nyuma ya *Zana*.
        - Hakikisha unawapa uhakika wa uzima wa milele kwa kuomba na kusoma **1 Yohana 5:11-12**.
        - Wakisema "Hapana," waulize kwa nini hawataki kuweka imani yao kwa Yesu. Fafanua mkanganyiko wowote nao kulingana na jibu lao.
- Ikibidi, tumia vifungu vinavyounga mkono kutoka kwa nukta #4 ndani ya zana.


8. Hongera mtu huyo kwa imani yake mpya katika Yesu. Waambie kwamba huu ni mwanzo wa maisha yao mapya na kwamba ungependa kukutana nao tena ili kuwasaidia kukua katika imani yao mpya katika Kristo.

- Omba kukutana nao siku inayofuata au haraka iwezekanavyo.
- Andika wakati na mahali kwenye *Zana*.
- Andika majina yao na wakati na mahali pa kukutana nao kwenye sehemu ya kubomoa. Hifadhi hii kwako mwenyewe.
- Mpe mtu huyo *Zana* na umwombe asome mambo ya ndani kabla hamjakutana tena.

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."*

Yoahna 3:16-18

**Kutoka kwa mistari hii, unajifunza nini kuhusu...**




FUNGA

**Sala ya imani:** *"Bwana Yesu, nakuhitaji. / Ninakiri kwako kwamba nimetenda dhambi dhidi yako na ninastahili hukumu ya milele. / Asante kwamba ulikufa na kufufuka ili kusamehe dhambi zangu zote. / Ninakuomba unisamehe na unipe uzima wa milele. Amina."*

**Je, kwa dhati uliweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele? Una nini sasa? (1 Yohana 5:11-12)**

Huu ni mwanzo wa maisha yako mapya na uhusiano wako na Mungu. Tungependa kukutana nawe tena ili kuzungumzia kutoka katika Biblia jinsi unavyoweza kukua katika uhusiano wako na Mungu. **Je, tunaweza kukutana lini kesho?**

Wakati ______________ Mahali ____________________________

FUNGA

Wakati ________ Mahali ____________

Vidokezo

---

Jina ______________________ Simu ________________

Anwani ____________________________________________

1. **Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele pamoja Naye.**
   - **2 Petro 3:9** - *"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*
   - **Warumi 5:8** - *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*
2. **All people are separated from God because of their sin.**
   - **Warumi 3:23** - *"... kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*
   - **Warumi 6:23** - *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."*
   - **2 Wathesalonike 1:8-9** -*Yesu atarudi... "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;."*
3. **Mungu alimtoa Mwanawe pekee mkamilifu ili afe badala yako ili kulipia dhambi zako.**
   - **2 Wakorintho 5:21** - *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*
   - **Yohana 14:6** - *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.'"*
4. **Ni lazima uamini (weka imani yako) kwa Yesu kama njia pekee ya kukusamehe dhambi zako na kupata uzima wa milele.**
   - **Yohana 1:12** - *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*
   - **Waefeso 2:8-9** - *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*
   - **Warumi 10:9-10** - *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*
5. **Ukimtumaini Yesu pekee kama mwokozi wako anakupa uzima wa milele.**
   - **1 Yohana 5:11-12** - *"... Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

www.StrategicImpactInternational.com

© Permission to copy with attribution


3 Arrows Hope & Life Tool v3.0

[Endelea kwenye ukurasa unaofuata]

# NANI?

Nani umshuhudie Injili rahisi kwa uwazi?
**KILA MTU** — lakini anza na wale ambao unamuunganiko nao.

1. Tumia jedwali hilo hapo chini ili **kuorodhesha** watu ambao unamuunganiko nao katika maisha ya **kila siku**. Miunganiko hii inaweza ikawa ya marafiki wa karibu au watu ambao munaonana mara kwa mara sokoni au maeneo mbalimbali, lakini huwajui majina yao.
2. Kwa muda wa wiki zima, **omba kila siku** kwamba Mungu afungue mioyo yao waisikie Injili.
3. **Tenga muda wa kuwaendea** (inaweza ikawa kwenye ratiba zako za kawaida) **washirikishe** mambo amabayo Mungu ameyafanya kwako, na washirikishe ujumbe rahisi wa Injili kwa kutumia *Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha ya SI*.




- Uwe makini na watu ambao Mungu anawaleta kwenye maisha yako **kila siku** ili uweze kuwashirikisha Injili.
- Omba na kupambanua **kundi** au **mahali** munapoweza kwenda kuhubiri Injili.

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 5 - *USHUHUDA WAKO BINAFS*

TIMU WATU 3-5 KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10 15 VITUO VYA MAPUMZIKO

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umejizuia dhidi ya mawazo ya ngono na matendo yake au je umezoelea tabia yoyote ambayo inaleta vifungo?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Matendo 26:1-29** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Matendo 26:1-29** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Ni mambo gani muhimu ambayo paulo alikuwa anasisitiza juu ya ushuhuda wake wa kuokoka?

7. Shirikisha jambo moja au mawili ambayo Yesu ameyafanya katika kubadilisha maisha yako tangu umeokoka?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI* 5 ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Matendo 26:1-29** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 5 - *USHUHUDA WAKO BINAFS*

Kila Mkristo kama Paulo, ana habari ya kusema (ushuhuda) wa namna alivyokutana na Yesu ushuhuda wako ni habari ya kipekee ya namna ulivyomwamini Yesu na jinsi alivyobadilisha maisha yako. Mungu atatumia ushuhuda wako kugusa watu wengine na kufungua mlango wa kuwaeleza wengine Injili.

Ili Mungu akutumie wewe ni muhimu sana ujihusishe na "watu wa nje" (Wakolosai 4:5) unapokutana na kuongea na watu wengine anza kwa kuwauliza juu ya hadithi "yao ya maisha." **Waulize maswali** kuhusu wanachoamini. Yafuatayo ni maswali ya mfano ambayo yatasaidia kujua uhusiano wa mtu na Mungu:

"Je unamwamini Mungu? Kwanini, au kwa nini humwamini?"

"Je unaweza kuuelezeaje uhusiano wako na Mungu? Je unajisikia upo karibu au mbalina Mungu au karibu na Mungu?"

"Unadhani ni kitu gani kinachokuzuia kuwa na uhusiano na Mungu? Unafikiri unaweza kufanya nini ili kuwa na uhusiano mkubwa na Mungu?"

"Je una hakika kwamba unao uzima wa milele na Mungu baaada ya kufa?"

"Kwa maoni yako unadhani Yesu Kristoni nani? Unadhani alikuja duniani kufanya nini?"

"Ni kitu gani ambacho Mungu anataka uwe na hakika kwamba unao uzima wa milele baada ya kufa?"

**Waombe ruhusa ili**, uwaeleze tofauti ambayo Yesu ameifanya kwenye maisha yako (Yaani ushuhuda wako). Habari yako lazima…

- **Iwe kwa ufupi** — isiwe Zaidi ya dakika moja (isizidi dakika 2) !
- **Yawe ni mazungumzo** — "usihubiri" au kutoa ujumbe, yawe ni mazungumzo tumia sauti ya mazungumzo. Siyo mambo ya kukariri.
- **Usitumie maneno ya kidini** au ya kitheolojia ambayo watu wanje hawayaelewi.
- **Usiongelee habari za kanisa lako** au mambo mengine yasiyo na umuhimu, maadili, siasa n.k.
- **Sema habari za Yesu** na mambo ambayo amefanya kwenye maisha yako!
- Zungumza juu ya **mambo matatu ya msingi:**
    1. Maisha yako yalivyokuwa kabla ya kukutana na Yesu…
    2. Jinsi ulivyokutana na Yesu…
    3. Tofauti ambayo Yesu aliifanya na anayoendelea kuifanya kwenye maisha yako…
- **Ushuhuda wako ubebe mambo ya msingi ya Injili** — kwa kusikiliza ushuhuda wako mtu aelewe jinsi anavyoweza kuokoka.
- **Malizia kwa swali/mwaliko wa kusikia tena habari za Mungu** "Je ungependa kujua jinsi ya kupokea uzima wa milele?"
- **Andika** (chambua na uhakiki) **lakini usikariri**. Baada ya kuandika ushuhuda wako, soma kwa mtu mwingine kisha upe maoni. Pitia na usome kwa sauti yako mwenyewe kwa siku 30.
- **Washirikishe wengine mara kwa mara ombea milango ya kushuhudia ifunguliwe!**

Kazi ya Kufanya: Andika ushuhuda wako mwenyewe kwa kufuata mwongozo huo hapo juu. Fuata mpangilio huu, **(1) Maisha yangu kabla ya kukutana na Yesu** (eleza jambo moja au mawili ambayo ni ya kweli kabla hujakutana na Yesu), **(2) Jinsi nilivyosikia na kumwamini Yesu**… **(3) Tofauti ambayo Yesu ameifanya kwenye maisha yangu**. (Jinsi Yesu alivyobadilisha jambo moja au mawili makubwa). Msomee mtu ambaye atakupa mrejesho baada ya kukusikiliza. Pita tena kisha soma tena kwa sauti kwa ajili yako mwenyewe kwa siku 30. Washirikishe watu wengine ushuhuda huu mara kwa mara!

**KWELI YA MSINGI:** MUNGU ATAUTUMIA USHUHUDA WAKO KUWASHAWISHI WATU WENGINE KUMWAMINI KRISTO.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 6 - *KIPAUMBELE CHA UPENDO*

**TIMU WATU 3-5** **KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10** **15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je ni nani ambaye umemuongeza kwenye *RAMANI YA HUDUMA* mwezi huu?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **1 Wakorintho 13:1-13** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **1 Wakorintho 13:1-13** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Unatakiwa upendo wa Yesu uumbike ndani yako. Unaposoma 1 Wakorintho 13:4-7 kwenye neno "upendo" weka jina lako katika kila usemi (mfano:"Israel ni mwema na mvumilivu") kama familia yako, marafiki majirani au maadui zako wakisikia ni usemi upi watakao uamini kuwa wa kweli?

7. Ni mabadiliko gani unayotakiwa kuyafanya kwenye maisha yako ili upendo uumbike kwenye mahusiano yake yote (familia, majirani, kanisani)?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 6* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **1 Wakorintho 13:1-13** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 6 - *KIPAUMBELE CHA UPENDO*

1 Wakorintho 12 inaeleza umuhimu wa karama za roho ambazo Mungu amewapa watu wake. Inaelekeza kuungana na Roho Mtakatifu hata kama kunatofauti ya karama. Munahitajiana pamoja na tofauti zilizopo ili mwili kamili wa Kristo uweze kudhihirishwa kwa utukufu wa Mungu. Umeelekezwa "kwa shauku kutamani karama zilizo kuu." KISHA, Biblia inakuambia kwamba kuna jambo lililo muhimu zaidi ya karama — ***"njia iliyo bora zaidi"*** (1 Wakorintho 12:31b). njia iliyo bora zaidi ni njia ya **UPENDO** iliyoelezwa ukurasa unaofuata wa kitabu cha Wakorintho.

1 Wakorintho 13 inajulikana sana — inajulikana kiasi kwamba maneno yake yamepoteza nguvu kwa kiasi Fulani. Zingatia jinsi umuhimu wa upendo ulivyolinganishwa na karama nyingine na uwezo katika mistari ya 1-3. Upendo ni kiungo kinachofanya karama na uwezo mwingine viwe na thamani. Bila upendo, karama na matendo mengine ni machukizo, hayana matunda na hayana thamani.

**SOMA: Mathayo 22:36-40**. Yesu akizingatia matamko ya torati na mafundisho na maelekezo ya manabii, vyote vinaeleza UPENDO — kumpa muda Mungu na kumpenda jirani yako vinashikamanishwa katika **UPENDO**.

1. Upendo ni **agizo** la msingi kutoka kwa Yesu Kristo (Mathayo 22:34-40; 1 Yohana 4:19-21; Mathayo 5:43-47). Mpende Mungu, mpende jirani yako. Huwezi kufanya moja bila kufanya lingine.
2. Upendo ni **ushahidi** wa kazi ya Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22-23). Tunda la Roho Mtakatifu ni UPENDO — unaodhihirisha furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhiri, uaminifu, upole na kiasi.
3. Upendo ni **uthibitisho** kwamba ni wafuasi wa Yesu Kristo (Yohana 13:34-35). — Yesu anampa KILA MTU — mwenye dhambi na Mtakatifu — haki ya kujihoji kama kweli wewe ni mwanafunzi wake kweli. Kipimo cha pekee ni **KUPENDANA** sisi kwa sisi.
4. Upendo ndio lengo la maelezo ya mafundisho na ulinzi dhidi ya upotofu wa mafundisho yasiyo na umuhimu au yenye uzushi tu (1 Timotheo 1:5).
5. Upendo unatakiwa kuwa **mzizi** la matendo yako yote (1 Corinthians 16:13-14). Jilinde! Simama imara! tenda kama wanaume halisi! — lakini "mambo **yote** uyatendayo yatende kwa upendo!"

Upendo unaonekanaje katika maisha ya kila siku? Jibu linapatikana katika 1 Wakorintho 13:4-13, uvumilivu, wema,kutokuwa na wivu au kujivuna kutokuwa na uchungu au karaha; kufurahi pamoja na kweli; kuamini, kutumaini, na kuvumilia yote.

Yesu akirudi, hutahitaji karama nyingi za Mungu.

**Unabii**? Utapita, kutakuwa na haja gani ya kutabiri mbele za uwepo wa Yesu?
**Lugha**? Zitakoma, utazihitaji kwa ajili ya nini?
**Maarifa**? Yatapita, kwakuwa utakuwa unajua kwa ukamilifu!
**Imani**? Imani yako itakuwa imetoshelezwa na itakuwa inaonekana!
**Tumaini**? Imani yako itakuwa imetimirika ndani ya nafsi ya Yesu Kristo!

**Upendo**, unadumu milele.

**KWELI YA MSINGI:** LAZIMA UPENDO UWE NDO KITOVU CHA MAMBO YOTE UNAYOFANYA KATIKA MAENEO YOTE YA MAISHA YAKO NA HUDUMA.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

## HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 7 - *MTINDO WAKO WA MAISHA YA UINJILISTI*

**TIMU WATU 3-5 KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10 15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata. Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Yohana 4:1-39** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Yohana 4:1-39** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Je ni nani ambaye waamini wanamkwepa na kutofuata mfano wa maisha yake kwa sababu ya kutokuwafikiria wengine kwa ajili ya Kristo?

7. Ni mipango gani binafsi ninayoweza kujiwekea ili nianze kuishi kwa kuitangaza Injili?

**[Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 7* ukurasa unaofuata.]**

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Yohana 4:1-39** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA______________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ______________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 7 - *MTINDO WAKO WA MAISHA YA UINJILISTI*

Ni fursa iliyoje na wajibu wa kuwashirikisha Injili ya Yesu Kristo watu waliotuzunguka. Injili pekee inaleta amani na Mungu na tumaini la uzima wa milele. Ni kwa njia ya kuiamini Injili mtu anapokea kipawa cha Mungu cha wokovu na kupata uzima, upendo wa ushirika na Mungu na watu wengine. Mtume Petro anakukumbusha juu ya fursa na wajibu wa kuwashirikisha wengine Injili kama mtindo wa maisha 1 Petro 3:15b – *"Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu,…"*

Petro anakuhimiza *"uwe tayari kutoa jibu."* Katika hadithi uliyosoma juu ya kukutana kwa Yesu na mwanamke kisimani, uligundua Yesu alikuwa tayari kushiriki Injili na alichukua hatua ya kufanya hivyo na watu alipokutana nao. Vivyo hivyo, katika mafunzo yako, umejifunza jinsi ya kushiriki vitu muhimu vya ujumbe wa Injili wazi na kwa kutumia tu *MISHALE 3 ZANA YA TUMAINI NA MAISHA YA SI*. Unapoendelea kutumia zana hii, utapata ujasiri zaidi na furaha katika kushiriki. Ukiwa na silaha na ushuhuda wako na kifaa hiki, na ukiongozwa na Roho Mtakatifu, kwa ujasiri utaanza mazungumzo ya kiroho na watu waliopotea ambao wanahitaji kusikia Habari Njema.

Petro anakutia moyo wewe kujiandaa kutoa majibu *"kwa kila mtu aulizaye."* Roho Mtakatifu yupo kazini wakati wote kuiandaa mioyo kuipokea Injili utakayowashirikisha. Anawahakikishia watu kwamba ni wenye dhambi na kuwasukuma kutafuta suluhisho kwa kujitenga kwao na Mungu. Yesu hakumshurutisha yule msamaria ili ajijue kuwa ni mwenye dhambi na kwamba anahitaji wokovu; badala yake, wajibu wako ni kuwashirikisha suluhisho la Mungu juu ya hitaji lao. Hii kweli ikupe ujasiri wa kuchukua hatua kwa uhuru kuwashirikisha Injili watu unaowafahamu na unaokutana nao. Hali ukijua kwamba Roho Mtakatifu amekwisha kuiandaa mioyo kuipokea kweli na amekuandaa wewe kupanda hiyo kweli kwenye mioyo yao. Wajibu wako ni kutafuta watu ambao wako tayari kupokea mambo ya kiroho. Kama vile Yesu, anzisha mazungumzo kwa kuuliza maswali na kuongea na watu katika maisha ya kila siku ili kuelewa kiwango cha shauku yao juu ya mambo ya rohoni.

Moja ya njia ambayo Roho Mtakatifu anaandaa mioyo ya watu wanaomhitaji Yesuili kupokea Injili ni kwa njia ya kutazama mabadiriko ya maisha yako. Hivi ndivyo Petro anavyomaanisha anaposema kwamba unatakiwa kujiandaa kumjibu kila mtu aulizaye kumpa *"sababu ya tumaini ulilonalo."* Watu wanakuangalia unavyoishi. Wanapoona kazi ya Roho Mtakatifu ya kubadirisha maisha kwako, watataka kujua ni jinsi gani na wao wanaweza kupata ulichonacho. Tumaini lako kwa Yesu linaambukiza na kuvutia!

Petro anaanza kwa kukutia moyo wewe "*ili kila wakati*" uwe tayari kuhubiri Injili. Uinjilisti ni zaidi ya tukio. Uinjilisti ni **mtindo wa maisha**. Uinjilisti ni kuliishi tumaini ulilonalo ndani ya Kristo ambalo linatoa mvuto wa ndani kwa watu waliokuzunguka ili waamini Injili unayoihubiri. Habari ya kazi ya Mungu kwenye maisha yako, ikiambatana na ushahidi wa Roho aliyekubadirisha inakuhusu wewe kuwaelezea wengine kwa urahisi, waziwazi na kwa ujasiri kwamba yale wanayoyaona kwako wanaweza wakayapata pia, kama wakiweka tumaini lao kwa Yesu.

Kwa hiyo, kaka na dada zangu, wakati wote jiandae kuchukua hatua ya kuwashirikisha wengine habari njema kwamba Yesu ni tumaini lako na yeye ndiye tumaini pekee la uzima wa milele katika Mungu.

**KWELI YA MSINGI:** YESU MARA ZOTE ALISHIRIKISHA UJUMBE WA KIPEKEE WA UZIMA WA MILELE, NA UNATAKIWA UMFUATE YEYE KWA KUPELEKA UJUMBE WA INJILI KWA KILA MTU KAMA MTINDO WA MAISHA.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 8 - *MSINGI WA BIBLIA*

**TIMU WATU 3-5** **KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10** **15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano yako na wenzio, majirani na maadui zako?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **2 Timotheo 3:14-17** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **2 Timotheo 3:14-17** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Kusudi la Mungu ni nini kukupa Biblia kwa ajili ya maisha yako?

7. Ni kwa njia ipi katika hizi 6 za kuishika Biblia ambayo wewe unahitaji ili kukua?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 8* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **2 Timotheo 3:14-17** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

**STRATEGIC IMPACT - SAFARI YA MAISHA KUFIKIA ULIMWENGU WAKO ULIOPOTEA**

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 8 - *MSINGI WA BIBLIA*

Msingi wa mafanikio ya maisha ya mkristo na huduma ni kuijua na kutii Biblia. Mungu alikupa Biblia *"ili uwe kamili, umeandaliwa kwa kila kazi njema"* (2 Timotheo 3:16-17). Huwezi ukakua katika imani na kuwahudumia wengine mpaka uijaze akili yako, moyo wako na mtindo wa maisha wa kweli ya Biblia. Biblia inaeleza njia sita unazoweza kuzitumia ili kupanda kweli ya neno kwenye maisha yako.

1. **Kusikiliza**. Wana wa Israel walikusanyika kusikiliza Biblia (Yoshua 8:34-35). Paulo alimwambia Timotheo kusoma Biblia hadharani (1 Timotheo 4:13). Mara kwa mara sikiliza wengine wakisoma, pengine kama familia. Kama ikiwezekana sikiliza Biblia za sauti au kwenye mitandao.


2. **Kusoma**. Kila mfalme wa Israel alijiandikia nakala yake ya Biblia *"aliisoma siku zote za maisha yake"* (Kumbukumbu la Torati 17:18-19). Kanisa limeagizwa kusoma nyaraka za Agano Jipya (Wakolosai 4:16). Lazima uendelee na kurudi kusoma Biblia yote. Tunakutia moyo kusoma sura tatu kila siku.

3. **Kujifunza**. Ezra *"alikuwa amejitoa kwa moyo wote, kujifunza na kushika sheria ya Bwana"* (Ezra 7:10). Kwa uangalifu angalia, tafsiri na tenda kama Biblia inavyosema ili uelewe inachofundisha, ili uweze kujifunza kuishi maisha ya haki (2 Timotheo 3:16-17).

4. **Kukariri**. kijana anaishi maisha matakatifu kwa kulificha neno la Biblia moyoni mwake (Zaburi 119:11). Yesu alisimama kinyume cha majaribu ya shetani kwa kukiri mistari ya Biblia ambayo alikuwa ameikariri (Mathayo 4:4, 7, 10). Tunakutia moyo kukariri angalau andiko moja kwa wiki Mbinu iliyothibitishwa katika hili ni kusoma hilo andiko kwa sauti mara saba kwa siku kwa siku saba.

5. **Kutafakari**. Mungu alimwambia Yoshua kutafakari Biblia usiku na mchana (Yoshua 1:8). Zaburi ya 1 inasema kwamba maisha yenye matunda na utele ni matokeo ya kutafakari Biblia. Kutafakari maana yake ni kufikiri kwa uangalifu jinsi ya kutendea kazi Biblia kwenye maisha yako. Kutafakari na kukariri vinaenda pamoja.

6. **Kutendea kazi na kutii**. Mungu amekupa Biblia ili kubadirisha maisha yako. Usipoitendea kazi kweli ya Biblia, Yakobo anasema unajidanganya mwenyewe (Yakobo 1:22-25).




Mkono wako ni njia nzuri ya kukumbuka hizi njia 6 za kupanda neno kwenye maisha yako. Vidole vinawakirisha njia za kushika Biblia, kiganja kinawakirisha utii.Kama utatendea kazi haya mambo sita utakuwa "umeshika" vizuri Biblia!

**KWELI YA MSINGI:** MSINGI WA MAISHA YA MKRISTO NA HUDUMA NI KUIELEWA NA KUTII BIBLIA.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

## Hatua 1 - Kituo cha Mapumziko 9 - *Ukiri wa Dhambi na Ushirika na Watu Wengine*

**Timu Watu 3-5** **Kuangalia Mambo 4 - Maswali 10** **15 Vituo vya Mapumziko**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *Maswali ya ya Kukua Kiroho* - ukurasa wa 6)

1. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo? Kwa namna gani?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *Kituo cha Mapumziko* kinachofuata. Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **1 Yohana 1:5-9** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **1 Yohana 1:5-9** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Ni huduma au shughuli gani za kidini ambazo unafanya zinazochukua nafasi ya ushirika wa upendo wako kwa Yesu?

7. Ni mambo gani ya vitendo yaliyokusaidia kukuza ushirika na upendo wako wa kwanza kwa Yesu?
[**Someni pamoja *Mwongozo wa Safari* 9 ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **1 Yohana 1:5-9** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***Kituo cha Mapumziko*** kinachofuata.

*Strategic Impact - Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 9 - *Ukiri wa Dhambi na Ushirika na Watu Wengine*

Ushirika na Mungu pamoja na watu wengine ni jambo muhimu sana. 1 Petro 3:18 inasema kwamba Kristo alikufa ili kukuleta wewe kwenye **ushirika na Mungu**. Yesu alisema kwamba *Hivyo watu wote watambue ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi"* (Yohana 13:35). Yesu anaupa ulimwengu ruhusa kuhukumu kama kweli wewe ni mfuasi wake kwa kuangalia ushirika wako na Mungu pamoja na sisi kwa sisi. Katika 1 Yohana 1:5-10 unaona mambo mawili yanayokinzana: **(1)** Kutembea katika nuru kunakinzana na kutembea katika giza, na **(2)** Kukiri kwamba umetenda dhambi kunakinzana na kukataa kwamba hujatenda dhambi.

**KUTEMBEA NURUNI**

Mungu ni Mtakatifu. Mungu ni nuru. Hajawahi kuwa gizani (dhambi) kwa kuwa giza ni kutokuwepo nuru. Ushirika wako na Mungu unategemea namna unavyotembea naye. Ushirika wako na Mungu haufunuliwi kwa maneno Yetu, bali kwa kile unachokifanya (mistari 6). Ukitembea gizani, huwezi kuwa na ushirika na Mungu. Lakini, kama ukienenda nuruni, kama ambavyo Mungu ni nuru, siyo tu kwamba utakuwa na ushirika na Mungu lakini utakuwa na ushirika na watu wengine pia, na dhambi zako zitasamehewa. Kutembea nuruni haimaanishi ukamilifu. Inamaanisha kuendelea vizuri kukua kiroho. Kuna vipindi utakanyaga giza na dhambi, lakini hupaswi kubakia huko. Endelea kukiri dhambi zako na kisha rejea kutembea kwenye nuru, kitu ambacho kinakupeleka UKINZANA wa pili.

**KUKIRI KWAMBA UMETENDA DHAMBI**

Biblia iko wazi inaposema kwamba *"wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"* (Warumi 3:23). Wakati Mwamini akiungama dhambi anarejeshwa kwenye ushirika na Mungu pamoja na watu wengine. Damu ya Kristo ina nguvu sana kiasi cha kusamehe dhambi YOYOTE. Mungu ambaye ni nuru, ana nguvu sana kiasi cha kushinda giza LOLOTE. Usisahau hata kidogo kuendelea kujitakasa.Unaweza kujivunia kuwa mwenye haki, kutegemea wema wako. Kuna hatari kwa wachungaji na viongozi wa kikristo kufikia hatua ya kukataa si kwamba hawatendi dhambi, lakini kudai kwamba hawajawahi kutenda dhambi. Wachungaji na washirika wote wako sawa katika kuitegemea damu ya Kristo kwa ajili ya msamaha wa dhambi. Wote munatakiwa kuenenda katika unyenyekevu na kuwa makini kuhusu dhambi katika maisha Yenu. Furahini kwamba Mungu ametukomboa sisi, na kwamba amekusamehe wewe na atakusamehe dhambi yeyote uliyonayo sasa, kama ukitubu. Kukataa kwamba hujatenda dhambi *"cani kumfanya Mungu kuwa muongo na kwamba neno lake halimo ndani yetu"* (1 Yohana 1:10). Lazima wakati wote kuendelea kuungama dhambi zako (kubaliana na kile Biblia inasema).

**MADHARA**

Ushirika na Mungu pamoja na watu wengine ni jambo tamu na lenye kupendeza katika maisha yetu na huduma. Kuharibu huo ushirika ni kujidhuru mwenyewe. Kama hatuwezi kuwa wakweli watu wengi hawatatuamini au kutusikiliza tunachosema kuhusu Kristo. Uaminifu katika kukiri au kuungama ndicho tunachokiomba na uaminifu katika kujibu *Maswali ya ya Kukua Kiroho* kila mara munapokutana katika timu ni jambo muhimu sana. Unapowajibika kwa Mungu na kwa kila mmoja, utakuwa katika neema yake, na utafurahia ushirika mzuri na Mungu pamoja na watu wengine ndani ya Kristo. Unapoungama dhambi zako wazi wazi kwa Mungu, yeye ni mwaminifu kusamehe. Ni pale tu unapopokea msamaha wa Mungu ndipo unapoweza kujifunza kusamehe na kuwapenda wengine. Ulimwengu unakuangalia kama wewe ni mkweli kuhusu dhambi zako mwenyewe. Watu wanakuangalia kama utaweza kusamehe kama wewe ulivyosamehewa. Ulimwengu unakutazama kama unafurahia ushirika wako na Mungu pamoja na wengine. ULIMWENGU UNAKUTAZAMA UNACHOKIONYESHA?

**Kweli ya Msingi:** MARA KWA MARA UNGAMA DHAMBI ZAKO ILI KUTUNZA USHIRIKA WAKO NA MUNGU PAMOJA NA WAAMINI WENGINE.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# Hatua 1 - Kituo cha Mapumziko 10 - *Kuwafanya Wanafunzi Waliokomaa na Wanaojizidisha*

**Timu Watu 3-5** **Kuangalia Mambo 4 - Maswali 10** **15 Vituo vya Mapumziko**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *Maswali ya ya Kukua Kiroho* - ukurasa wa 6)

1. Je umekuwa na kiasi na kumheshimu Kristo kwenye michakato yako ya kifedha?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *Kituo cha Mapumziko* kinachofuata. Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Marko 1:16-17** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Marko 1:16-17** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Elezea wanafunzi waliokomaa na wanaojizidisha wanaonekanaje?

7. Unatakiwa kuwaje ili kuwafanya waamini wengi kuwa wafuasi wa Yesu waliokomaa?

[**Someni pamoja *Mwongozo wa Safari 10* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Marko 1:16-17** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***Kituo cha Mapumziko*** kinachofuata.

### *Strategic Impact - Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 10 - *Kuwafanya Wanafunzi Waliokomaa na Wanaojizidisha*

Agizo Kuu la Kristo lipo wazi: *"nendeni mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi"* (Mathayo 28:19). Haitoshi tu kufanya uinjilisti unatakiwa utengeneze wanafunzi wanaojizidisha na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Wanafunzi wanapojizidisha makanisa mengi yatapandwa na kujizidisha. Agano jipya inafunua viwango vinne vya kuwaandaa wanafunzi wanaokuwa na kujizidisha:

**Hatua ya kwanza** ni kumleta mtu amwamini Yesu. Hatua ya kwanza ya mwanafunzi ni **kuamini** (1 Yohana 5:11; 1 Wathesalonike 1:7-8). Jambo la kusikitisha ni kwamba, mara nyingi tunaishia hapo. Unawaalika watu wamwamini Kristo na kisha kuwaambia wajiunge na kanisa halafu hatufanyi jambo lingine kuwasaidia. Waamini wapya ni watoto wachanga ndani ya Kristo wanahitaji kuangaliwa ili wakue! (1 Wakorintho 3:1-2; 1 Petro 2:2). Ni muhimu sana katika hatua hii wewe kama mwalimu au mlezi kuwa na muda na waongofu wapya ili kuwasaidia kukua. Yesu alifanya hivyo kwa wale ambao kwanza waliweka imani zao kwake. (Yohana 1:35-42).

Katika **hatua ya pili** unamsaidia mwamini kuwa **mfuasi** wa Kristo (Marko 1:17; Yohana 1:43; Wakolosai 2:6-7). Mfuasi wa Kristo anaelewa na kuitumikia kweli ya msingi kama hakika ya wokovu, jinsi ya kuhusiana na Roho Mtakatifu, umuhimu wa ubatizo na kanisa, jinsi ya kuungama dhambi, jinsi ya kuomba. *Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI* itakuongoza kusaidia na wengine kugundua na kufanya haya. Ni muhimu pia **kuwaonyesha jinsi** ya kufanya mambo haya. Wanatakiwa wakuone wewe ukiishi kweli. Kwa hiyo katika hatua hii wajibu wako ni **KUDHIHIRISHA** jinsi ya kumfuata Kristo (1 Corinthians 11:1-2; 2 Timothy 3:10-11). Wanafunzi wa Yesu walijifunza kwa kumtazama Yesu akiomba, akishuhudia, akiwajali wagonjwa na maskini na kuwafundisha Biblia. Na sisi pia, ni lazima tuwaelekeze na kuwaonyesha wengine jinsi ya kuishi ndani ya Kristo **na** kumtumikia.

**Hatua ya tatu** ni kumsaidia mfuasi wa Kristo kuwa **mtenda kazi** wa Kristo, (Waefeso 4:12). Yesu aliwaambia wanafunzi wake, *"Nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu,"* (Marko 1:17). Mfuasi "anavua" watu. Wafuasi wote wanatakiwa wafundishwe kuhubiri Injili na kuwasaidia wakristo wapya kukua ndani ya Kristo kutumia *Mishale 3 Zana ya Tumaini na Maisha* na *Uanafunzi ya Strategic Impact*. Waefeso 4:12 inasema kwamba wafuasi wanatakiwa kuandaliwa ili kufanya kazi ya huduma kuwapenda na kuwatumikia wengine. Waite ili **waongozane na wewe** unapoenda kufanya huduma. Wajibu wako ni **KUKASIMU** wajibu wa huduma kwa wafuasi wako unapowatazama na kuwafundisha (Mathayo 10; Luka 10).

**Hatua ya nne** ya kuwafanya wengine kuwa wanafunzi ni kumsaidia mtenda kazi ili **kujizidisha**, (Mathayo 9:36-37; 28:18-20; Yohana 15:5,16). Kujizidisha ndiyo shabaha yako. Utakuwa umetimiza wajibu wako ikiwa wanafunzi wako wameanza kuwafundisha wengine (2 Timotheo 2:2). Utaendelea kuwatia moyo na kuwasaidia, lakini kwa sasa watakuwa **na wajibu kamili wanawajibika** kuzaa wengine na kuwafanya kuwa wanafunzi. Ni pale tu ambapo watu uliowaleta kwa Kristo na wanapoanza na wao kuwaleta watu wengine katika imani kwa Kristo na kuwafundisha wengine na kuwasaidia kupanda makanisa hapo unaweza kusema umefanikiwa (Matendo 6:1, 7). Wajibu wako wa msingi kwa hawa wanaozaa ni kuwafanya **WAJIZIDISHE**. Ni muhimu kwako kushiriki kwenye *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*, lakini pia **kuwafundisha wengine** kutumia mafundisho haya.

Omba na kufanya kazi ili uone **waamini** wakiwa **wafuasi** ambao watakuwa watenda kazi ambao **watajizidisha** (Wakolosai 1:28-29). Lakini hatua hizi hazitokei kwa mpangilio kama vile moja baada ya nyingine, hatua zote zinatokea **wakati mmoja**. Waamini wapya wanapokua wasaidie waanze kutumika na kuanza kujizidisha mchakato huu unapojirudia, mtembeo wa kasi utatokea katika mji wote, taifa na kanda na AGANO JIPYA litatimizwa.

**Kweli ya Msingi:** SHABAHA YAKO NI KUWAFANYA WANAFUNZI WALIO AMINI, KUWA WAFUASI WATENDA KAZI NA WANAOJIZIDISHA.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# Hatua 1 - Kituo cha Mapumziko 11 - *Kushirikiana na Roho Mtakatifu kwa Njia Sahihi*

**Timu Watu 3-5** **Kuangalia Mambo 4 - Maswali 10** **15 Vituo vya Mapumziko**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *Maswali ya ya Kukua Kiroho* - ukurasa wa 6)

1. Je umejizuia dhidi ya mawazo ya ngono na matendo yake au je umezoelea tabia yoyote ambayo inaleta vifungo?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *Kituo cha Mapumziko* kinachofuata. Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Matendo 1:8 na Wagalatia 5:16-22** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Matendo 1:8 na Wagalatia 5:16-22** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Ni jinsi gani Roho Mtakatifu anakuwezesha kuishi kwa ajili ya Kristo na kumtumikia?

7. Ufanye nini ili kutembea katika nguvu za Roho Mtakatifu?

[**Someni pamoja *Mwongozo wa Safari 11* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Matendo 1:8 na Wagalatia 5:16-22** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***Kituo cha Mapumziko*** kinachofuata.

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 11 - "*Kushirikiana na Roho Mtakatifu kwa Njia Sahihi*"

Mungu ana shauku ya kuona unakuwa na USHIRIKIANO ULIO HAI NA YESU KRISTO kwa njia ya Roho Mtakatifu anayeishi ndani yako (Warumi 8:9-14). Mungu hajawahi kukukusudia wewe umtumikie kwa jitihada zako mwenyewe. Amekupa Roho wake ili kwamba uweze kukua ufanane na Kristo na umtumikie kwa nguvu zake. Anafanya haya unapotembea katika Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:16). Mambo haya yanamaanisha nini?

**Kwanza**, Roho Mtakatifu **atakufariji na kukutia moyo** (Yohana 14:15-21). Yeye ni mshauri wako. Atakufariji moyoni na katika akili ili ufurahie faraja yake ni lazima **utii** maagizo yake (Yohana 15:14-15).

**Mbili**, Roho Mtakatifu **atakuongoza kwenye kweli yote** (Yohana 16:12-15). **Aliwavuvia** mitume wa kwanza kuandika Biblia, Neno la Mungu lililofunuliwa. Sasa **analiweka wazi** kupitia maneno ya kwenye Biblia (Waefeso 1:17-18). Lazima usome Biblia kwa **kusikiliza sauti ya Roho Mtakatifu, unaposoma omba**, **"Bwana sema nami."**

**Tatu**, Roho Mtakatifu **atazaa tena maisha ya Yesu ndani yako** (2 Wakorintho 3:18). Ulipomwamini Yesu, Roho wake alikuja kukaa ndani yako (2 Wakorintho 5:17). Kuzaliwa upya haimaanishi kwamba umekwisha komaa ndani ya Kristo, ingawa Roho Mtakatifu ataendelea kukubadilisha tabia ili ufanane na Yesu. Hili ni tunda la Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22-23). Anafanya hivi unapochagua kila **siku kusema "Ndiyo" kwake** na hapana kwa shauku ya mwili.

**Nne**, Roho Mtakatifu atakuongoza **kufanya na kusema anachotaka** (Warumi 8:14; Wagalatia 5:21; Wafilipi 2:12-13). Atakusukuma kuwa na shauku na kutenda kwa namna ambayo utampendeza yeye. Anaongea na moyo na akili yako, lakini unapaswa kuwa mwangalifu kwa kuwa shetani naye anaweza kushawishi mawazo yako. **Uwe makini kwa msukumo wa Roho Mtakatifu katika nyakati tofauti tofauti, lakini hakikisha kwamba uongozi wowote unaopewa unaendana na Biblia.**

**Tano**, Roho Mtakatifu **atawapata waongofu wapya kuwafundisha kuwa wanafunzi kupitia wewe** (Yohana 15:26-27; Matendo 1:8; 1 Petro 4:10-11). Huwezi ukafanya kazi hii ya Kiungu kwa uwezo wako mwenyewe, lakini utakapokuwa unashuhudia wengine Roho Mtakatifu atawavuta wengi katika imani ndani ya Kristo. Atatumia karama za Roho anazokupa ili kuwasaidia waamini wengine kukaa katika imani. Kwa **hiyo shiriki na Roho Mtakatifu kwa kuwaambia wengine habari za Yesu** na tarajia atafanya kazi ndani yako na kupitia wewe kuwasaidia wengine kukua.

Yesu alikupa Roho wake ili kukufariji, kukufundisha, kukubadilisha, kukuongoza na kupitia wewe ili kuwapata wengine kwa ajili ya Yesu. Utakuwa na maisha ya furaha na yenye matunda utakapokuwa unashirikiana na Roho Mtakatifu na kutembea naye hatua kwa hatua kila siku.

**Kweli ya Msingi:** MUNGU ALIKUPA WEWE ROHO MTAKATIFU ILI AKUHUDUMIE NA KUPITIA WEWE UNAPOSHIRIKIANA NAE KWA UKAMILIFU.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 12 - *MUHIMU KWA KUWAFUNDISHA WENGINE*

**TIMU WATU 3-5** **KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10** **15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je ni nani ambaye umemuongeza kwenye *RAMANI YA HUDUMA* mwezi huu?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **2 Timotheo 1:2-3, 14; 3:10-17** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **2 Timotheo 1:2-3, 14; 3:10-17** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Ni zana gani ambazo Mungu anazitumia ili kuwasaidia wengine kukua na kuwafanya wanafunzi waliokomaa?

7. Ni watu gani hao wawili ambao Mungu anataka uanze kuwafundisha kwa kukusudia?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 12* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **2 Timotheo 1:2-3, 14; 3:10-17** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10.Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 12 - *MUHIMU KWA KUWAFUNDISHA WENGINE*

Wito wako ni kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha ambao wataanzisha makanisa yanayojizidisha. Unapohubiri Injili kwa uaminifu, watu wengi watamwamini Kristo kama Mwokozi. Ni muhimu sana kuwasaidia kukua na kuwa wanafunzi wanaojizidisha watembelee watu majumbani kwao, shuleni na mahali pao pa kazi. Wafundishe waamini wapya pekee yao au kwenye kikundi cha watu wa 3-5, kama ikiwezekana mtembelee mwamini mpya ndani ya masaa 48 baada ya kumwamini Kristo. Wapatie Injili ya Yohana kama unayo. Tumia mwongozo wa **Topiki 4 au Safari 4 za Kutembelea** waongofu wapya. Muongozo unapatikana kwenye kipeperushi au *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*. Baada ya kumtembelea safari ya kwanza, panga naye ratiba ya kukutana naye kila wiki hadi umalize Safari 4 za Msingi.

### Mambo muhimu ya ufuatiliaji na *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*

Kuwasaidia waamini kukua na kuwa wanafunzi wanaojizidisha kunahusisha mambo mengi kuliko tu kujifunza Biblia. Mambo yafuatayo ni zana muhimu kwa ajili ya kuwafundisha wengine:

1. **Biblia** ni "mtaala"muhimu sana unaweza kuutumia kufundisha wengine (2 Timotheo 3:16-17)!
2. **Omba kwa uaminifu** kwa ajili ya na pamoja na waongofu wapya (Waefeso 1:15-23).
3. Watie moyo waamini wapya kumtegemea **Roho Mtakatifu** ili kuwabadilisha wafanane na Kristo (2 Wakorintho 3:17-18).
4. **Wewe!** Ushawishi wako kwa waamini wapya ni muhimu. Tenga muda wa kuwa na waamini wapya mbali na ule muda wa kujifunza Biblia. Wachukue unapoenda kuwashuhudia wengine wacha "waone" unavyomfuata Yesu katika maisha yako ya kila siku (2 Timotheo 3:10-11).

Baada ya Safari 4 za kwanza za kuwatembelea waamini wapya, waulize wale ambao walikuwa waaminifu kupatikana uwaombe kuwatembelea tena Safari 20 zingine zaidi. Wasaidie kujizidisha kwa: **(1)** Kujifunza Biblia na namna ya kumfuata Yesu (**Kukua**); **(2)** Waonyeshe jinsi ya kumweleza mtu mwingine habari za Yesu (**Ushuhudiaji**); **(3)** Watie moyo kutumia zana hizi kwa wanafunzi wengine (**Kujizidisha**).

### Mutakapokutana pamoja fuata mchakato huu wa Hatua 5

1. **MAHUSIANO**: Waulize wanaendeleaje na tafuta yaliyojiri katika maisha yao tangu mlipoachana kwenye mkutano wenu wa mwisho.

2. **KUTIA MOYO**: Anza kipindi kwa kujibu *MASWALI YA KUKUA KIROHO* (yanayotokana na Wagalatia 5:22-23): **Wiki hii…**
   A. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?
   B. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano na familia, marafiki, waamini wenzio, majirani na maadui zako?
   C. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo Wiki hii? Kwa namna gani?
   D. Je umekuwa na kiasi na kumheshimu Kristo kwenye michakato yako ya kifedha?
   E. Je umejizuia dhidi ya mawazo ya ngono na matendo yake au je umezoelea tabia yoyote ambayo inaleta vifungo?
   F. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?
   G. Je umekuwa mwaminifu kusoma Biblia na kutimiza mambo **mliyokubaliana kufanya** wiki hii?

3. **KUJADILIANA**: Someni na mjadiliane vifungu vya Biblia vilivyoainishwa katika kila safari kwa kutumia **Maswali 6** (kama ilivyoelekezwa kwenye *Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI*)
4. **MPANGO**: Kubalianeni maandiko ya kwenye Biblia ambayo kila mtuatasoma wiki hii. (tunashauri Sura 3 kwa siku).
5. **OMBA**: Malizia muda wa kukutana nao kwa maombi ya pamoja mkiombeana kila mtu na mwenzie na kuombea mipango mliofikia kutokana na Maswali ya 5 na 6.

**Kweli ya Msingi:** ZANA MUHIMU ZA KUWAFUNDISHIA WENGINE NI BIBLIA, MAOMBI, ROHO MTAKATIFU, NA WEWE.

[**Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"**]

**KUMBUKA**: Maelezo kamili ya *Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI* inapatikana ukurasa wa 49-50.
Uwe huru kutoa nakala unazohitaji kwa matumizi kwa gharama zako kwa ajili ya kutumia kwenye uinjilisti.

## ZANA KWA KITUO CHA MAPUMZIKO 12 - *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*

### Fuata Hatua 5 Za Maendeleo Ya Msingi Munapokutana pamoja

1. **MAHUSIANO**: Waulize wanaendeleaje na tafuta yaliyojiri katika maisha yao tangu mlipoachana kwenye mkutano wenu wa mwisho.

2. **KUTIA MOYO**: Anza kipindi kwa kujibu ***MASWALI YA YA KUKUA KIROHO*** (yanayotokana na Wagalatia 5:22-23): **Wiki hii…**
   a. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?
   b. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano na familia, marafiki, waamini wenzio, majirani na maadui zako?
   c. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo Wiki hii? Kwa namna gani?
   d. Je umekuwa na kiasi na kumheshimu Kristo kwenye michakato yako ya kifedha?
   e. Je umejizuia dhidi ya mawazo ya ngono na matendo yake au je umezoelea tabia yoyote ambayo inaleta vifungo?
   f. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?
   g. Je umekuwa mwaminifu kusoma Biblia na kutimiza mambo **mliyokubaliana kufanya** wiki hii?

3. **KUJADILIANA**: Someni na mjadiliane vifungu vya Biblia vilivyoainishwa katika kila safari kwa kutumia **Maswali 6** (kama ilivyoelekezwa kwenye *ZANA YA UKUAJI NA KUZIDISHA YA SI*)
   a. Hakikisha kila mtu anajisikia vizuri kujadiliana maswali kwa kufuata Biblia. [**ZINGATIA**: Hapa **sio** mahali pakutoa ujumbe. unawasaidia waamini wapya namna wanavyoweza kujifunza Biblia kwenye maisha **yao**.]

**MASWALI 6**

Mmoja na asome kifungu husika kwa sauti wakati wengine wanasikiliza au wanasoma wakifuatilia tokea kwenye Biblia.

Uliza maswali mawili ya awali na waruhusu waendelee kujadiliana na kupeana mawazo:

1. *Umepanda nini kutoka kwenye kifungu hiki?*
2. *Kitu gani hujapenda, au umeona kina changanya, kuhusiana na habari au kifungu hiki?*

Kusoma kifungu tena. Kujadili ijayo maswali mawili:

3. *Je, wewe kujifunza kuhusu watu kutoka katika kifungu hiki?*
4. *Je, wewe kujifunza kuhusu Mungu kutoka katika kifungu hiki?*

Baada ya muda wa majadiliano, mmoja asome kifungu kile kwa mara ya tatu kwa sauti na kisha jadilianeni maswali ya mwisho:

5. *Kulingana na kifungu hiki maisha yako yanawezaje kubadilika wiki hii? Uwe dhahili tambua. (Andika majibu ya watu na kisha mtakapokutana tena waulize maendeleo yao kulingana na majibu yao haya.)*
6. *Unamfahamu na mwingine anayehita kujua hadithi au kifungu hiki? (Taja jina, na sema kwa nini na lini utakapo mshirikisha au kumwambia.)*

b. Pitia **somo** la **Safari 1**: “Yesu ni nani?” na maandiko yake Yohana 14:1-11.

c. Ukimaliza somo la kwanza somo la kutembelea safari 1, wewe na waamini wapya mutakuwa muyasoma mafungu ya maandiko hayo ya Biblia **mara 3**.

d. Ninyi nyote mtakuwa mmejibu maswali yote ya kwanza 4 ambayo yatakuwa yamewasaidia.

e. Ninyi nyote mutakuwa mumejitoa kutii kutenda makubaliano kutokana namlivyojifunza kuwashirikisha wengine habari za Yesu.

f. f) Katika safari inayofuatamuwe na uhakika wa kufuatilia kila mmoja kulingana na namna mlivyotii na kutimizamakubaliano mliyoyafanya kwenye swali la 5 na lile la 6 la kujitoa kufanya uinjilisti.

## <u>Ziara za Msingi</u>

**<u>1:</u>** Yesu ni nani?
*Yohana 14:1-11*

**<u>2:</u>** Maisha Mapya na Upendo wa Mungu.
*Yohana 3:1-18*

**<u>3:</u>** Uwe na uhakika wa wokovu wako.
*Yohana 10:27-30*

**<u>4:</u>** Kukaa ndani ya Yesu.
*Yohana 15:1-11*

g. Kuna topiki zingine tatu na maandiko yaliyotolewa kama **Safari ya Msingi** kwa wanafunzi wa baadae. Ni muhimu kukumbuka kwamba lengo ni kuwasaidia waamini wapya kuweza kusoma, kuelewa na kuitii Biblia wakiwa wenyewe wanapoendelea kukua katika uhusiano wao na Yesu na waamini wengine.

h. Baada ya **Safari nne za Msingi**, ni wakati mzuri kutulia na kufanya tathimini ya maendeleo ya waamini wapya na kufanya maamuzi ya kuendelea na **Safari za Kuwasaidia Kukua** kiroho au la. Kama wamekuwa waaminifu kuendelea kukutana, na wamekuwa katika uaminifu wa kutunza kwa uaminifu kutekeleza makubaliano ya kila wiki, na kama wamemshirikisha mtu mwingine habari za Yesu, hapo unaweza kuendela kuwafundisha masomo ya kukua kiroho na kisha uwalete kanisani

4. **MPANGO**: Kubalianeni maandiko ya kwenye Biblia ambayo kila mtuatasoma wiki hii. (tunashauri Sura 3 kwa siku).
   a. Uwe makini kwa wale wasiojua kusoma.
   b. Wapatie Biblia ya sauti kama ipo.
   c. Hakikisha unaandika kwenye karatasi majibu kutokana na Swali la 5 na 6 ili kufuatilia kwenye safari ya kutembelea inayofuata.
   d. Panga safari inayofuata ya kuwatembelea wanafunzi.
   e. Angalia wale waliotayari kushiriki na waliojitoa kusoma nyumbani na kujifunza zaidi kuhusu Kristo na kuwashuhudia wengine habari za Yesu. Hawa ndo watu unaotakiwa kuendelea nao kuwafundisha na kuhusiana nao hata baada ya kuwatembea Safari 4.

5. **OMBA**: Malizia muda wa kukutana nao kwa maombi ya pamoja mkiombeana kila mtu na mwenzie na kuombea mipango mliofikia kutokana na Maswali ya 5 na 6.

# Hatua 1 - Kituo cha Mapumziko 13 - *Ubwana wa Yesu*

**Timu Watu 3-5** **Kuangalia Mambo 4 - Maswali 10** **15 Vituo vya Mapumziko**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *Maswali ya ya Kukua Kiroho* - ukurasa wa 6)

1. Je umejikabidhi kwa Roho Mtakatifu na kutunza upendo wenye shauku kwa ajili ya Yesu?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *Kituo cha Mapumziko* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **Marko 8:27-38** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **Marko 8:27-38** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Wewe unatoa jibu gani kwa swali la Yesu, "Ninyi mnasema Mimi ni Nani?

7. Elezea ni kwa jinsi gani utajikana kwa ajili ya Yesu na Injili.

[**Someni pamoja *Mwongozo wa Safari 13* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **Marko 8:27-38** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***Kituo cha Mapumziko*** kinachofuata.

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 13 - *Ubwana wa Yesu*

Yesu aliwauliza wanafunzi wake (na sisi) maswali mawili muhimu (Marko 8:27-38). Majibu yako kwa haya maswali yataamua **hatima yako ya milele** na **vipaumbele vyako**.

Swali la **kwanza** linaloulizwa Yesu ni nani? Katika siku za maisha yake duniani watu walikuwa na maoni tofauti tofauti kumhusu Yeye. Wengine walidhani ni Yohana Mbatizaji, au Eliya au mmoja wa manabii. Watu wengi hata hii leo wanadhani ni kiongozi mkubwa wa dini au mtu mwadilifu wa mfano, lakini Yesu anatuuliza sisi,***"Na ninyi mnasema yakuwa Mimi ni nani?"*** (mstari 29). Jibu pekee lililokubalika ni lile alilolitoa Petro: "*Wewe ndiwe Kristo!*" ukiri wa Petro unathibitisha kwamba Yesu ni Masia Mwana pekee wa Mungu wa milele, aliyefanyika kuwa mwanadamu na alikufa, kwa ajili ya kutusamehe dhambi. Ni Bwana mfufuka ambaye atarudi duniani ili kumhukumu kila mtu na kisha atatawala milele. Hatima yako ya milele inategemea unamwamini Yesu kama nani.

Swali la pili muhimu linapatikana kwenye mafundisho aliyotoa Yesu baada ya ukiri wa Petro. Yesu alitabiri juu ya mateso yake, kifo na kufufuka kwake kisha akatoa haya maelekezo kwa kila anayemsikiliza.

> *"Ndipo akawaita wale watu pamoja na wanafunzi wake aka waambia, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwe nyewe, auchukue msalaba wake, anifuate. Kwa maana mtu ye yote aipotezaye nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya kuitangaza Habari Njema, ataiokoa. Mtu atafaidi nini kama atapata ulimwengu wote lakini akayaangamiza maisha yake? Au mtu atatoa nini apate tena maisha yake? Mtu ye yote atakayenionea aibu mimi na maneno yangu katika kizazi hiki kiovu na kisichomjali Mungu, na mimi, Mwana wa Adamu, nitamwonea aibu wakati nitakapokuja katika utu kufu wa Baba yangu na malaika watakatifu."* (Marko 8:34-38).

Swali la **pili** linasema kwamba, **"Unaishi hapa duniani kwa ajili ya nani?"** Una uchaguzi wa aina mbili tu: unaweza ukaishi kwa makusudi yako binafsi na kupata raha zote za dhambi ambazo hutolewa na ulimwengu wa uovu, au unaweza kupoteza maisha yako kwa ajili ya Kristo na Injili.

Ingawa ni jambo la kawaida kufikiri ni vizuri kuishi kwa yale unayoyapenda na kupata mambo mengi kadri utakavyo Yesu anasema mwisho wa siku "utapoteza" nafsi yako ile kweli yako ya kiroho. Wewe ni zaidi ya mwili, huu wa muda. Wewe una umilele, roho na nafsi zetu zimeumbwa na muumba kwa ajili ya makusudi yake.

Uchaguzi mzuri ni kuishi kwa ajili ya Yesu Kristo na Injili yake. Unapomfuata kwa ujasiri na kuishi kwa ajili ya Injili yake, utaipata nafsi yako — ile furaha na hali ya kiroho uliyoumbiwa na sifa na thawabu kutoka kwa Yesu utakazopata atakaporudi. (Mstari 38)

**Kweli ya Msingi:** KUJIKANA MAMBO BINAFSI KWA AJILI YA KRISTO, MWANA WA MUNGU WA MILELE, NA INJILI KUTASABABISHA MAISHA MAZURI.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

# HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 14 - *WAKATI WAKO PEKE YAKO NA MUNGU*

TIMU WATU 3-5 KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10 15 VITUO VYA MAPUMZIKO

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umetembea katika upendo, amani, wema na msamaha katika mahusiano yako na wenzio, majirani na maadui zako?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**
Soma kwa sauti **Marko 1:21-39 na Luka 5:15-16** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**
Soma tena **Marko 1:21-39 na Luka 5:15-16** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Kwa nini unadhani Yesu aliweka kipaumbele cha kujitenga ili kuwa na muda wa pekee yake na Baba yake?

7. Ni mabadiliko gani utakayoyafanya ili kuufanya muda wako ni Mungu kuwa kipaumbele?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 14* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**
Soma tena **Marko 1:21-39 na Luka 5:15-16** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**
Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# Hatua 1 - Mwongozo wa Safari 14 - *Wakati Wako Peke Yako na Mungu*

Muda wa pekee yako na Mungu wa kila siku ni muhimu kwa ajili yako ili kukua katika upendo na kumtii Kristo, kuifanya upya akili yako, kuangalia mbele na kuhamasika kukaa kwenye kweli ya wito wako.

Hivi ndivyo walivyofanya watumishi wa Mungu wakubwa wanaume na wanawake, kwenye Biblia na katika historia. Kuwa na Muda endelevu na Mungu, kusoma na kujifunza Biblia na kuomba ni muhimu kwa ajili ya kukua kama mtoto na mtumishi wa Mungu. Bila hivyo huwezi kufurahia uhusiano wako na Mungu wako ambao ndiyo shauku yake kwako.

Yesu alidhihirisha jambo hili katika maisha yake mwenyewe. Kama muda wa kuwa na Mungu kila siku ulikuwa muhimu kwake — Asiyekuwa na dhambi, Mwana wa Mungu mwenye nguvu zote – je ni kwa kiasi gani sisi watoto wa Mungu dhaifu, Wenye dhambi, na wahitaji tunahitaji kuwa na Muda wa pekee yetu na Mungu!

Mumejadili huduma ndefu "ya siku" ya Yesu katika Marko 1:21-39, iliyoanza mapema alipofundisha kwenye sinagogi na kuendelea hadi usiku akifundisha na kuponya. Pamoja na hayo kama kipaumbele Yesu alianza mapema asubuhi siku iliyofuata alikuwa na muda na Mungu. Sura hii ikienda sambamba na Luka 5:15-16, inatufundisha mambo 4 ambayo Yesu alifanya:

1. Kuwa na Mungu Baba yake kwa njia ya maombi, kutafakari Biblia na kusikiliza uongozi wa Roho Mtakatifu Yesu aliviweka kuwa kipaumbele.
2. Alipanga kuwa na Muda — aliamka asubuhi na mapema (katika Marko) na akajitenga mwenyewe ili kuomba (Luka).
3. Alijitenga na watu ili kuwa na muda wa pekee yake na Baba yake.
4. Alikwenda mahali Fulani (Sehemu maalumu).

Ni lazima ufuate mfano wa Yesu kama unataka kutunza ushirika wako na Mungu ulio hai na kuwa na huduma yenye ufanisi kwa Kristo. Baadhi ya mambo ambayo waamini wameona yana msaada ni pamoja na: Kurekodi kwenye kitabu mawazo, maombi na mambo ambayo Mungu amekuwa akiwafundisha; kusoma kijitabu cha ibada kinasaidia, kuimba na kuabudu, Bwana; na kutenga muda fulani kwa kufunga, kuomba na kutafakari.

Kumbuka, kwamba kuwa na Muda pekee yako na Mungu siyo kwa ajili ya huduma kwa wengine au kufanya maandalizi ya masomo, bali ni kwa ajili ya kukuza ushirika wako na Mungu.

**Kweli ya Msingi:** KUWA NA MUDA WA PEKEE YAKO NA MUNGU KWA SIKU NI MUHIMU KAMA UNATAKA KUKUA KWENYE UHUSIANO WAKO NA MUNGU.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

## HATUA 1 - KITUO CHA MAPUMZIKO 15 - *JINSI YA KUJIFUNZA BIBLIA*

**TIMU WATU 3-5** **KUANGALIA MAMBO 4 - MASWALI 10** **15 VITUO VYA MAPUMZIKO**

**ANGALIA NYUMA** (Pitia *MASWALI YA YA KUKUA KIROHO* - ukurasa wa 6)

1. Je umekuwa katika upendo na ibada kwa ajili ya Kristo? Kwa namna gani?

2. Je, ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi ya "NITAFANYA" wiki hii?

3. Je umekuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafundisha wengine? Nani hao?

[**KUMBUKA**: kama mmoja wenu hajatekeleza kipengele cha makubaliano ya mambo ya KUFANYA, basi msiendelea mbele! Kila mtu lazima atekeleze alichosema NITAFANYA kabla ya kwenda kwenye *KITUO CHA MAPUMZIKO* kinachofuata.
Kama jambo hili linatokea mara kwa mara rejea ukurasa wa 6 kwa msaada Zaidi.]

**ANGALIA JUU**

Soma kwa sauti **2 Timotheo 3:14-17 na Ezra 7:10** kisha jadilianeni maswali yafuatayo.

4. Ni kitu gani ulichokipenda au kilichokutia moyo kwenye maandiko haya?

5. Ni kitu gani kimekuchanganya au kimekufanya ujisikie vibaya kwenye maandiko haya?

**ANGALIA NDANI**

Soma tena **2 Timotheo 3:14-17 na Ezra 7:10** kisha jadilianeni maswali yafuatayo...

6. Mistari hii inaeleza matokeo gani yatatokea ikiwa utajua na kuelew vizuri na kuitii Biblia?

7. Kwa nini unadhani ni muhimu sana kwa mtu kuwa mwanafunzi wa maisha wa Biblia?

[**Someni pamoja *MWONGOZO WA SAFARI 15* ukurasa unaofuata.**]

**ANGALIA MBELE**

Soma tena **2 Timotheo 3:14-17 na Ezra 7:10** kisha jadilianeni...

8. Katika mwangaza wa hii mistari ni jambo gani la utii **utakalofanya** wiki hii ? Eleza kitu maalumu.

   "NITAFANYA________________________________________________"

9. Ni nani utakaye mshirikisha habari za Yesu na kumfundisha wiki hii ? (Zana zipo ukurasa wa 47-50)

   Majina: ________________________________________________

   Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kazi pamoja ya uinjilisti na kufundisha waongofu wapya wiki hii?

10. Ni fungu gani la Biblia utakalosoma wiki hii ? (Tunashauri sura 3 kwa siku)

**MAOMBI**

Munapohitimisha ombeaneni juu ya mahitaji yenu na endeleeni kuyakabidhi maombi hayo kwa Bwana mpaka mutakapokutana ***KITUO CHA MAPUMZIKO*** kinachofuata.

# HATUA 1 - MWONGOZO WA SAFARI 15 - *JINSI YA KUJIFUNZA BIBLIA*

Shabaha ya huduma yako ni kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha hadi Kizazi cha 4 (Angalia 2 Timotheo 2:2). Paulo alimfundisha Timotheo ambaye alitakiwa kufundisha watu wengine waaminifu. Moja ya "nyenzo" muhimu ambayo Paulo aliitumia ni kumfundisha Timotheo kweli ambayo yeye alijifunza kwa Yesu (Soma 2 Timotheo 1:13-14; 22, 15; 3:10, 14).

Paulo kwa msisitizo alimwambia Timotheo kuendelea katika yale aliyojifunza na pia kutoka katika "Maandiko Matakatifu" (2 Timotheo 3:14-15). Kisha akaeleza sababu kwamba; : *"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate* ***kutenda kila tendo jema****"* (mistari 16-17).

Kama munataka kukua na kuwa wanaume na wanawake ambao Mungu anataka muwe, lazima ujifunze **kujua**, **kuelewa**, na **kuthamini** Biblia kwenye maisha yako. Kama unataka kufanya wanafunzi wanaojizidisha lazima utumie Biblia ili kuwasaidia kukua na kuwa wanaume na wanawake waliokomaa katika Mungu Ezra ni mfano mzuri kwetu *"alikuwa ameuelekeza moyo wake kuitafuta sheria ya Bwana, na kuitenda na kufundisha maagizo na hukumu katika Israel."* (Ezra 7:10).

Kila mmoja wenu anatakiwa kutengeneza ujuzi wa kujifunza Biblia. Ujuzi huu utakuwezesha wewe kuwa mwanafunzi wa maisha wa Biblia, anayeelewa, anayeishi na kuwafundisha wengine.

Kuna **hatua tatu za msingi** katika kujifunza Biblia:

1. Lazima **uone** kitu ambacho Biblia inasema. Hii inamaanisha **kutazamak** wa uangalifu kilichoandikwa.
   Mara nyingi hatujawa waangalifu ili kuona waziwazi kitu ambacho mwandishi wa Biblia ameandika. Kuangalia kilichoandikwa ni kusoma kwa uangalifu na kwa kurudia rudia ili uone kitu ambacho Biblia inasema.

2. Lazima **uelewe** Biblia inachomaanisha. Hii ni **kutafsiri** kilichoandikwa.
   Tafsiri sahihi ya Biblia inakuja pale ambapo unakuwa umeelewa maana ya asili ya mwandishi kwa wakati alioandika na kwa watu aliowaandikia ujumbe.

3. Lazima **utendee kazi/kuyatumia** mafundisho ya Biblia. Hii inamaanisha **uyaweke kwenye matendo mambo** yaliyoandikwa.
   Jambo muhimu katika kujifunza Biblia nikwa kutafakari kwa makini jinsi gani maandiko **yanavyoweza kutumika** kwenye maisha yako. Mungu anataka utendee kazi kweli ambayo umeigundua. Mungu hajakupa Biblia kwa ajili ya taarifa tu. Anataka maisha yako yabadirishwe na kweli yake.

Mwongozo *BINAFSI ZANA WA KUJIFUNZA BIBLIA* utakusaidia kuangalia, kuelewa na kutendea kazi Biblia kwenye maisha yako.

(Anzeni kwa kila *TIMU YA SAFARI* kutumia zana hii kujifunza 2 Timotheo 2:1-7 wiki hii.)

**KWELI YA MSINGI:** LAZIMA UWE MWANAFUNZI WA MAISHA WA BIBLIA ILI UJUE INACHOSEMA, UTII KWELI YAKE NA UWAFUNDISHE WENGINE KUFANYA HIVYO.

**[Rudi ukurasa wa nyuma kujadiliana kipengele cha "ANGALIA MBELE"]**

## MWONGOZO BINAFSI WA KUJIFUNZA BIBLIA

Maandiko: ________________________________ Tarehe: ______________

### ANGALIA: Unaona NINI?

| | |
|---|---|
| Ninajifunza **nini** kuhusu Mungu, Yesu, na Roho Mtakatifu? | Ni watu **gani** wanaosemwa kwenye mistari hii? Ninajifunza nini mimi au watu? |
| Kuna **ahadi** na **maagizo** gani kwenye andiko? | Kitu gani kinachosababisha tatizo litokee? Mambo **yanahusianaje**? |
| **Lini** na **wapi** jambo hili lilitokea? Eleza mahali na wakati au mazingira | Ni maneno au wazo gani **muhimu** limekuwa **likijirudia rudia**? |
| **Kwa nini** mwandishi ameandika haya? Wasomaji walikuwa wamekabiliwa na tatizo gani? | Hii mistari inamaanisha nini kwenye hii sura? Je! Ni mada **kuu** au **wazo gani** la kifungu hiki? |

**KUMBUKA**: Kadri unavyotumia muda mwingi kuangalia andiko, ndivyo itakuwa rahisi kuelewa na kutafsiri hilo andiko.

**KUTAFSIRI: Majibu Ninayohitaji ili KUELEWA sura hii.**

| Maswali | Majibu |
|---|---|
| Dhana au neno gani la msingi ninalotakiwa kufafanua? | |
| Ni watu gani ambao wapo kwenye sura hii ambao natakiwa kujua taarifa zao zaidi? | |
| Mlingano au ukinzani gani ninaotakiwa kuelewa? | |
| Je kuna usemi wa mafumbo? Huo usemi una maana gani? | |
| Hii ni fasihi ya aina gani? (masimulizi ya kistoria, mashairi, torati, nyaraka, unabii) | |
| Je! Habari hii inahusiana vipi na mpango wa Mungu wa wokovu? (Agano la Kale, Agano Jipya) | |
| **Je! Ni nini ukweli wa msingi au wazo la kifungu hiki?** Andika jibu kwa sentensi moja tu. | |

**KUTENDA KAZI: Ni jinsi gani maandiko haya YATABADIRI KUFIKIRI KWANGU, MTAZAMO NA MATENDO YANGU?**

| Kufundisha | Kukemea | Kusahihisha | Kuadibisha Katika Haki |
|---|---|---|---|
| Kwa **mfano** wowote wa kufuata? Nimejifunza nini? Je kuna kanuni yoyote ya jumla ya namna Mungu anavyotenda au namna ninavyotakiwa kutenda? | Je kuna **dhambi** ninayotakiwa kutubu? Ni uongo upi ambao nimeuamini au mambo gani ninayokosea? Kwa nini? Mzizi wa mawazo haya ni upi? | Je kuna **agizo** lolote ninalotakiwa kufuata au kutii? Nitafanyaje sasa? Nitasahihishaje kufikiria kwangu vibaya na matendo yangu? | Je kuna **ahadi** yoyote ninayotakiwa kudai? Je naweza kuboresha vipi hili eneo kwenye maisha yangu? Je nitatengenezaje tabia au mazoea mapya ya kufikiri na kutenda? |


Sasa ni wakati wa kuongea na Mungu kuhusu mambo uliyojifunza na kile kitu ambacho Mungu **anataka utende leo**. Andika anachosema na mwitikio wako:

| **"...ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."** |
|---|
| |

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.”*

Yoahna 3:16-18

**Kutoka kwa mistari hii, unajifunza nini kuhusu...**




FUNGA

**Sala ya imani:** *“Bwana Yesu, nakuhitaji. / Ninakiri kwako kwamba nimetenda dhambi dhidi yako na ninastahili hukumu ya milele. / Asante kwamba ulikufa na kufufuka ili kusamehe dhambi zangu zote. / Ninakuomba unisamehe na unipe uzima wa milele. Amina.”*

**Je, kwa dhati uliweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele? Una nini sasa? (1 Yohana 5:11-12)**

Huu ni mwanzo wa maisha yako mapya na uhusiano wako na Mungu. Tungependa kukutana nawe tena ili kuzungumzia kutoka katika Biblia jinsi unavyoweza kukua katika uhusiano wako na Mungu. **Je, tunaweza kukutana lini kesho?**

Wakati ______________ Mahali ____________________________

FUNGA


Wakati __________ Mahali ____________________

Vidokezo

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.”*

Yoahna 3:16-18

**Kutoka kwa mistari hii, unajifunza nini kuhusu...**




FUNGA

**Sala ya imani:** *“Bwana Yesu, nakuhitaji. / Ninakiri kwako kwamba nimetenda dhambi dhidi yako na ninastahili hukumu ya milele. / Asante kwamba ulikufa na kufufuka ili kusamehe dhambi zangu zote. / Ninakuomba unisamehe na unipe uzima wa milele. Amina.”*

**Je, kwa dhati uliweka imani yako kwa Yesu kukusamehe dhambi zako na kukupa uzima wa milele? Una nini sasa? (1 Yohana 5:11-12)**

Huu ni mwanzo wa maisha yako mapya na uhusiano wako na Mungu. Tungependa kukutana nawe tena ili kuzungumzia kutoka katika Biblia jinsi unavyoweza kukua katika uhusiano wako na Mungu. **Je, tunaweza kukutana lini kesho?**

Wakati ______________ Mahali ____________________________

FUNGA

Wakati __________ Mahali ____________________

Vidokezo

Jina ______________________ Simu ________________

Anwani ____________________________________________

**1. Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele pamoja Naye.**

- **2 Petro 3:9** - *"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*
- **Warumi 5:8** - *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*

**2. All people are separated from God because of their sin.**

- **Warumi 3:23** - *"… kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*
- **Warumi 6:23** - *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."*
- **2 Wathesalonike 1:8-9** -*Yesu atarudi… "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;."*

**3. Mungu alimtoa Mwanawe pekee mkamilifu ili afe badala yako ili kulipia dhambi zako.**

- **2 Wakorintho 5:21** - *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*
- **Yohana 14:6** - *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.'"*

**4. Ni lazima uamini (weka imani yako) kwa Yesu kama njia pekee ya kukusamehe dhambi zako na kupata uzima wa milele.**

- **Yohana 1:12** - *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*
- **Waefeso 2:8-9** - *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*
- **Warumi 10:9-10** - *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

**5. Ukimtumaini Yesu pekee kama mwokozi wako anakupa uzima wa milele.**

- **1 Yohana 5:11-12** - *"… Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

www.StrategicImpactInternational.com
© Permission to copy with attribution
3 Arrows Hope & Life Tool v3.0

Jina ______________________ Simu ________________

Anwani ____________________________________________

**1. Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele pamoja Naye.**

- **2 Petro 3:9** - *"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*
- **Warumi 5:8** - *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*

**2. All people are separated from God because of their sin.**

- **Warumi 3:23** - *"… kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*
- **Warumi 6:23** - *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."*
- **2 Wathesalonike 1:8-9** -*Yesu atarudi… "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;."*

**3. Mungu alimtoa Mwanawe pekee mkamilifu ili afe badala yako ili kulipia dhambi zako.**

- **2 Wakorintho 5:21** - *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*
- **Yohana 14:6** - *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.'"*

**4. Ni lazima uamini (weka imani yako) kwa Yesu kama njia pekee ya kukusamehe dhambi zako na kupata uzima wa milele.**

- **Yohana 1:12** - *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*
- **Waefeso 2:8-9** - *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*
- **Warumi 10:9-10** - *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

**5. Ukimtumaini Yesu pekee kama mwokozi wako anakupa uzima wa milele.**

- **1 Yohana 5:11-12** - *"… Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."*

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL

www.StrategicImpactInternational.com
© Permission to copy with attribution
3 Arrows Hope & Life Tool v3.0

# SI

# Zana ya Ukuaji na Kuzidisha

V3.0

STRATEGIC IMPACT INTERNATIONAL
S.L.P. 78640 · Dar es Salaam, Tanzania
www.StrategicImpactInternational.com
© Jisikie huru kunakili na SI inayohusishwa

# Hatua 5

1. **HUSIKA**: Waulize wanaendeleaje na tafuta yaliyojiri katika maisha yao tangu mlipo achana kwenye mkutano wenu wa mwisho.
2. **TIA MOYO**: Anza muda wako kujibu maswali ya Ukuaji wa Kiroho (kulingana na Wagalatia 5: 22-23). **Wiki hii…**
   - A. *Je! Umejitiisha kwa Roho Mtakatifu na kudumisha upendo wa shauku kwa Yesu?*
   - B. *Je! Umetembea kwa upendo, amani, uvumilivu, fadhili, na msamaha katika uhusiano wako na familia, marafiki, waamini wenzako, majirani, na maadui?*
   - C. *Je! Umekua katika upendo wako na kujitolea kwa Kristo wiki hii? Vipi?*
   - D. *Je! Ulijidhibiti na kumheshimu Kristo katika shughuli zako za kifedha?*
   - E. *Je! Ulijidhibiti mwenyewe juu ya mawazo na matendo ya ngono, na tabia yoyote ya uraibu?*
   - F. *Je! Ulikuwa mwaminifu kuwashuhudia waliopotea na kuwafuata wengine? WHO?*
   - G. *Je! Ulikuwa mwaminifu kukamilisha usomaji wako wa Biblia na ahadi za "NITATAKA" wiki hii?*
3. **JADILI**: Soma na jadili kifungu cha Biblia mlichokuwa mmepeana mlipokutana kwa kufuata mfumo wa maswali 6 yafuatayo.
4. **MPANGO**: Pataneni kipengele cha maandiko matakatifu mtakayosoma wiki ijalo. (imependekezwa sura 3 kwa siku).
5. **OMBA**: Malizia muda wenu wa kukutana kwa maombi ya pamoja mkiombeana kila mtu na mwenzie na kuomba mipango mlioifikia kutokana na mswali va 5 na 6.

# Maswali 6

Mmoja na asome kifungu husika kwa sauti wakati wengine wanasikiliza au wanasoma wakifuatilia tokea kwenye Biblia.

Uliza maswali mawili ya awali na waruhusu waendelee kujadiliana na kupeana mawazo:

1. *Umepanda nini kutoka kwenye kifungu hiki?*
2. *Kitu gani hujapenda, au umeona kina changanya, kuhusiana na habari au kifungu hiki?*

Kusoma kifungu tena. Kujadili ijayo maswali mawili:

3. *Je, wewe kujifunza kuhusu watu kutoka katika kifungu hiki?*
4. *Je, wewe kujifunza kuhusu Mungu kutoka katika kifungu hiki?*

Baada ya muda wa majadiliano, mmoja asome kifungu kile kwa mara ya tatu kwa sauti na kisha jadilianeni maswali ya mwisho:

5. *Kulingana na kifungu hiki maisha yako yanawezaje kubadilika wiki hii? Uwe dhahili tambua. (Andika majibu ya watu na kisha mtakapokutana tena waulize maendeleo yao kulingana na majibu yao haya.)*
6. *Unamfahamu na mwingine anayehita kujua hadithi au kifungu hiki? (Taja jina, na sema kwa nini na lini utakapo mshirikisha au kumwambia.)*

# Ziara za Msingi

**1:** Yesu ni nani?
*Yohana 14:1-11*

**2:** Maisha Mapya na Upendo wa Mungu.
*Yohana 3:1-18*

**3:** Uwe na uhakika wa wokovu wako.
*Yohana 10:27-30*

**4:** Kukaa ndani ya Yesu.
*Yohana 15:1-11*

## Ziara za Ukuaji na Kuzidisha

**5:** Maombi.
*Mathayo 6:5-15*

**6:** Kiri dhambi zako na kutubia.
*1 Yohana 1:5 - 2:2*

**7:** Ushuhuda wako: Waambie wengine jinsi Yesu alivyokubadilisha.
*Matendo 26*

A. Tumia hizo pointi 3 zilizoonyeshwa hapa chini fikiria kupitia ushuhuda wako mwenyewe:
   1. *Maisha yangu yalikuwaje kabla hujamwamini Yesu.*
   2. *Jinsi mlivyokutana na Yesu.*
   3. *Tofauti Yesu aliyoifanya ndani ya maisha yangu tangu nilipo mwamini Yesu.*

B. Wape na wao kushuhudia angalau dakika moja na mtu kabla hamja kutana tena safari inayokuja.

**8:** Shuhudia: Waambie wengine habari za Yesu.
*Matendo 1:1-11*
*2 Wakorintho 5:16-21*

A. Wawezeshe kutumia nyenzo za Uinjilisti za SI.
B. Nenda nao kumwambia mtu habari za Yesu kwa kutumia nyenzo hizo.
C. TAMBUA: *Kama watawaongoza watu kwa Kristo wasaidie wajifunze namna ya kutumia mwongozo ili kuwawezesha kuwafundisha na kuwalea wale walioamini wapya.*

**9:** Jiunge kwenye faragha.
*Matendo 2:40-47*
*Waebrania 10:19-25*

A. Karibisha mfuasi mwanafunzi wako kuhudhuria seli au kanisa la nyumb la nyumbani.
B. Msaidie huyu mwanafunzi kujithibitisha kuwa mshiriki wa seli.

**10:** Ubatizwe.
*Matendo 8:26-38*
*Mathayo 28:19*
*Matendo 2:40-41*

A. Karibisha mwamini mpya apate kubatizwa.
B. Mpatie nafasi mwamini huyo mpya kukaribisha familia na marafiki *(hasa wale wasio mjua Kristo)* ili washuhudie ubatizo wake.

**11:** Meza ya Bwana.
*Luka 22:14-20*

A. Mkaribishe mwamini mgeni ashiriki pamoja na wewe na wengine meza ya Bwana.

**12:** Utii.
*Yohana 14:15-21*

A. Waulize ni eneo gani la maisha wanahisi Bwana anawauliza watu.

---

**13:** Muda wa faragha, Maombi, kusoma na kujifunza Biblia.
*Luka 5:15-16*

A. Mfanye mwamni mpya atenge muda kila siku wa kusoma Biblia na kuomba.

**14:** Wasamehe wengine.
*Mathayo 18:21-35*

A. Waulize Kama kuna mtu maalumu wanayepaswa kumsamehe.

**15:** Nyenyekea kwenye Ubwana wa Kristo kunyenyekea kuna uhuru wa siri ya Mungu.
*Warumi 14:5-12*

**16:** Makusudi ya Mungu juu ya maisha yako.
*Mathayo 28:18-20*
*2 Wakorintho 5:17-21*

**17:** Injili ni nini?
*1 Wakorintho 15:1-8*

**18:** Ndoa na Familia.
*Efeso 5:22 - 6:4*

**19:** Tembea katika Roho Mtakatifu.
*Wagalatia 5:16-26*

**20:** Utambulisho wake katika Kristo.
*Warumi 6*

**21:** Kipaumbele cha upendo.
*1 Yohana 4:7-21*

**22:** Mamlaka ya neno la Mungu.
*2 Timotheo 3:14-17*

**23:** Uwakili wa maisha.
*Luka 19:10-27*

**24:** Vita vya kiroho.
*Efeso 6:10-18*

# Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea
# *Hatua 1* kwa Ufupi

**HONGERA!** Sasa umemaliza *Hatua 1* of your *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*. Katika hatua hii umekuwa kwenye uhusiano wako na Yesu pamoja na watu wengine kwenye *Timu ya Safari*. Munafanya kazi pamoja ya uinjilisti na kuwafundisha waamini wapya. Kwa wakati huu kila mmoja anapaswa kuwa na **kikundi cha angalau wewe mwenyewe na wengine wawili** ambao unaongoza kupitia *Zana ya Ukuaji na Kuzidisha ya SI* "kutembelea."

Majina ya hao watu unaowafundisha unatakiwa uyaandike kwenye *Ramani ya Huduma* (ukurasa 5). Utaendelea kuwafundisha na kuwashauri ili nao wawe wanafunzi wanaozidisha. Lengo lako ni kuwafanya waanze kufanya wanafunzi ambao hufanya wanafunzi - kwa Kizazi cha 4. Kila mmoja wao anapaswa pia kupewa *Ramani ya Huduma* kuwasaidia kuanza. Wakati *Ramani ya Huduma* imekamilika hadi Kizazi cha 4, basi utaendelea kuwatia moyo na kuwashauri… na kisha anza nyingine *Ramani ya Huduma*!

Agizo Kuu ambalo Yesu alikupa linasema, *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…" (*Mathayo 28:18). Huu wito wa agizo ni kwa ajili ya **kila** Mkristo. Katika *Strategic Impact* tunaamini kwamba **tunachotakiwa kufanya ili kutimiza Agizo Kuu la Kristo ni kuendelea kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha hadi Kizazi cha 4.**

Huu ndo wito wako wa *Safari ya Maisha*. *Safari* Safari yako isikome labda kama utaenda kuwa na Bwana Mbinguni au Bwana atakaporudi. Utakapoendelea kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha, utakuwa na mguso wakujizidisha kunakotokana na kuwekeza kwenye maisha yao — NA kwenye maisha ya vizazi vya kiroho vya wanaojizidisha! Hakuna kitu unachoweza kukifanya katika maisha haya kama kuwafanya wanafunzi wanaojizidisha.

Sasa ni wakati wako wa kusonga mbele hadi **hatua inayofuata** ya *Safari* — kuendelea kufanya wanafunzi wanaozidisha **NA kuhusika katika kuanzisha na kuongoza kanisa jipya**. Kumbuka, kanisa ni **"kundi la wafuasi wa Kristo linaloongozwa na viongozi wa kiroho wanaostahili chini ya mamlaka ya Biblia ambao hukusanyika kwa ukawaida ili kumwabudu Mungu, kukua kiroho, kupendana na kutumikiana, na kwenda kufanya wanafunzi wanaozidisha kuongezeka katika ulimwengu wao uliopotea."** Inaweza kukutana katika nyumba, chini ya mti, kwenye uwanja wa mpira, katika chumba cha shule, au katika jengo lake. Mpangilio sio kile kinachofafanua kanisa.

Tunakualika uanze *Hatua ya 2* ya *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*. Katika *Hatua ya 2* utaendelea kukutana na *Timu yako* ya *Safari* ili kushiriki katika "***Kituo cha Mapumziko***" vya kila wiki, na pia kufanya kazi pamoja ili **kupanda** na **kuongoza kanisa jipya**. Lengo lako halitakuwa tu kufanya wanafunzi wengi zaidi bali ni kuongoza na kuanza **kuzidisha makanisa** unapowaongoza wengine katika *Hatua ya 1* ya *Safari*.

Mungu akubariki unavyoendelea na *Safari ya Maisha Kufikia Ulimwengu Wako Uliopotea*!

*Timu ya Strategic Impact*

**STRATEGIC IMPACT**
**S.L.P. 78640, DAR ES SALAAM, TANZANIA**
WWW.STRATEGICIMPACTINTERNATIONAL.COM
© Haki zote zimehifadhiwa na, Strategic Impact. Hakuna mabadiliko yanayoruhusiwa kwenye kitabu wiki, lakini unaweza kutoa nakala na kuwagawia wengine bila kubadili yaliyomo.